





**Atiwa** mbaroni kwa tuhuma za kuiba kichanga, mumewe ahojiwa

UKURASA 7


Nipashe Spotika
FIRMINO UK. 12-13
MBAPPE
WACHEZAJI 5 WALIOFUNGA HAT-TRICK NYINGI 2022
ISIKUPITE

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Januari 23, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581199

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# HUJUMA HIFADHINI

• **Majaji**, mahakimu watajwa, korti yaketi hadi Jumapili... *Endelea uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### RC AAGIZA MSAKO NYUMBA KWA NYUMBA WASIORIPOTI SHULENI



MKUU wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, amewaagiza viongozi na watendaji wote kuanzia ngazi ya mitaa kuwasaka nyumba kwa nyumba watoto wote ambao wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, lakini hadi sasa hawajaripoti shuleni...

UKURASA WA 3

### KINA CHA MAJI BWAWA LA NYERERE CHAFIKIA MITA 116

KINA cha maji kwenye bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere (JNHPP) kimefikia mita za uzajo 116 kutoka usawa wa bahari, ikiwa ni mwezi mmoja tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipofungua rasmi lango la kuchepusha maji na kuruhusu yajae bwawani...

## Mwenyekiti wa kijiji atuhumiwa kuuza mlima

UKURASA 4



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (katikati), akishiriki matembezi ya kilomita tano ya uzinduzi wa Wiki ya Sheria yaliyofanyika jijini Dodoma jana. Kushoto kwake ni Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Kamati Kuu ACT yatoa maazimio hoja nyeti

UKURASA 2

**MICHEZO** AZAM YAMREJESHA EDINHO IVORY COAST UK.20 **KABWELA** UK.7

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Charles Makongoro Nyerere (katikati), akifurahia jambo na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mirerani Benjamin William Mkapa alipofanya ziara ya kukagua wanafunzi walioripoti shuleni juzi, (kushoto) ni Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera na Mwalimu Mkuu, Samwel Kaitira (kulia). **PICHA: GIFT THADEY**

# Hujuma hifadhini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema baadhi ya mahakimu, majaji na mawakili wanashiriki kuhujumu maeneo ya hifadhi kwa kupokea rushwa na kuathiri utoaji haki.

Amesema hujuma hizo zinajumuisha mahakama kuzuia minada ya mifugo inayokamatwa kwenye maeneo hayo na kuwatoza faini ndogo wamiliki wa mifugo.

Akizindua Wiki ya Sheria kwenye Viwanja vya Nyerere Square jijini hapo jana, Makamu wa Rais alisema: “Katika ziara zangu ninazofanya mikoani na nyingine zinanikuta ofisini, ninapokea malalamiko mengi ya wananchi kuhusu mhimili wa mahakama lakini na vyombo vingine - polisi na magereza yenyewe, kwenye mfumo wa utendaji na utoaji haki kwa ujumla wake.

“Baadhi ya malalamiko ninayosikia ni kwamba baadhi ya mahakimu, mawakili na majaji sio waaminifu, wanadai rushwa kinyume cha kiapo chao, kuna minada ya mifugo ambayo inakamatwa kwenye maeneo ya hifadhi, mara kadhaa Mbeya kule tunaletewa malalamiko minada hiyo inazuiliwa kwa amri ya mahakama.

“Tena wakati mwingine unashtuka kabisa hiyo mahakama inakaa Jumapili au basi hizo faini ambazo zinaamriwa ni ndogo mno, kwa hiyo mwenye mifugo yake analipa faini baada ya nusu saa anarudisha mifugo yake kwenye hifadhi.”

Pia alisema amepokea malalamiko ya fedha za kigeni zinazokamatwa mipakani, zinapotea mikononi mwa mahakama na hukumu zinapindishwa ili kumpa ushindi mwenye fedha.

“Yapo malalamiko mengine, ni pamoja na gharama kubwa za uendeshaji wa kesi na kulipa gharama za mawakili, wananchi wanalalamikia hukumu kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza lakini pia watuhumiwa wanakaa mahabusu muda mrefu wanasubiri uchunguzi kukamilika.

“Wananchi wengine wanasema ‘jamani hatuna elimu ya sheria’, hivyo kuna ukosefu wa elimu ya sheria kwa umma pamoja na jitihada zote ambazo mmefanya,” alisema.

Aliwataka wahusika katika mfumo wa utoaji wa haki kuendelea kutoa elimu kwa umma na kuhakikisha huduma mbadala ya usuluhishi inapatikana na kufikika kwa urahisi.

“Nitoe wito kwa mahakama kushirikiana vyema na wadau katika kuimarisha utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi ili kufikia malengo yake kirahisi,” aliagiza.

Makamu wa Rais alisema mawakili wa kujitegemea wanapaswa kujielekeza katika kutoa elimu na ushauri sahihi kwa wateja wao kuhusu namna bora ya kutatua migogoro ikiwa ni pamoja na kutumia njia mbadala ya usuluhishi badala ya kuendelea na kesi mahakamani.

“Asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali yaendelee kutoa elimu kwa umma, misaada kwa wananchi na kujenga uelewa kuhusu haki za msingi za kiraia na umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi, pia viongozi wa dini na viongozi wa mila kote nchini wasaidie mahakama kuzungumza na wananchi kuhusu umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi,” alielekeza.

Pia aliagiza kuangaliwa upya ufanyaji kazi wa mabaraza ya ardhi nchini kutokana na kuongezeka kwa migogoro ya ardhi inayokosa usuluhishi wa mapema.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma, alitoa rai kwa wananchi wanaohitaji kudai haki zao, kufahamu kwanza haki hizo kwa kusoma na kutafuta elimu itakayowezesha kufahamu sheria na taratibu zinazoongoza haki inayotafutwa.

Alisema Wiki ya Sheria itatumika katika kutoa elimu na kuwakumbusha wananchi namna ya kupata haki zao kwa njia sahihi na rahisi.

Alisema wananchi wana wajibu wa kumaliza mashauri kwa njia ya usuluhishi huku akitoa wito kwa wananchi kutembelea Maonesho ya Wiki ya Sheria na hususani Mahakama Kuu Kituo cha Usuluhishi ili kupata elimu na uelewa zaidi kuhusu njia hiyo iliyosheheni faida lukuki kwa kuwa kufanya hivyo kutawapa nafasi ya kufanya shughuli za uzalishaji na kujiongezea kipato.

“Ni muhimu wananchi wafahamu pia namna ambavyo migogoro ya biashara, kazi au mikataba inayoweza kutokea kwa njia za mitandao,” alisema.

Maonyesho hayo yaliyozinduliwa jana yatafanyika kwa siku nane hadi Januari 29 yatajapohitimishwa yakifuatwa na kilele cha Siku ya Sheria itakayofanyika Februari Mosi mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan akiwa mgeni rasmi.


**KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI**

**SADICK W. CHIBUGA** anatangaza kupoteza kadi ya bajaji yenye usajili wa **MC 708DDT.** Kwa yeyote atakayeziona atoe taarifa polisi.

Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **IRI/IRI/RB/26552/2023.**



IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE
AT KOROGWE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.17 OF 2022
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE BONIFACE MHINA
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATIX
BY ELIZABETH WILLIAM SHEWAI

GENERAL CITATION
(MADE UNDER RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 03 Day of February, 2023

Date at Korogwe this 19 day of January , 2022


# Kamati Kuu ACT yatoa maazimio ya hoja nyeti

**Na Elizabeth Zaya**

KAMATI Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo kupitia kikao chake maalum imefikia maazimio mbalimbali na kutoa maelekezo kwa serikali.

Kamati hiyo imefikia maazimio hayo kupitia kikao chake kilichofanyika Januari 21 mwaka huu mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, alisema miongoni mwa maazimio hayo ni kutoa maelekezo kwa kamati ya wasemaji wa kisekta wa chama hicho kufanya uchambuzi wa kina wa hali ya kiuchumi na hatua za kuchukua kuukwamua.

Mengine kwa mujibu wa Shaibu ni pamoja na kutoa maelekezo kwa kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe kukamilisha uundwaji wa kamati ya kuisimamia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), ili kuiwajibisha na kupaza sauti dhidi ya hali ngumu ya maisha inayowakabili wananchi wa Zanzibar.

Azimio lingine kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, ni kuitaka SMZ kuweka wazi kalenda ya utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti ya vikosi kazi vya demokrasia.

Lingine ni kuitaka serikali kuweka wazi muda wa kuanza kwa mchakato wa Katiba Mpya hususani hatua muhimu za kupitiwa upya kwa sheria ya mabadiliko ya katiba hiyo pamoja na sheria ya kura ya maoni, kuitishwa kwa mkutano wa majadiliano ya kitaifa kuhusu Katiba, kuundwa kwa kamati ya wataalamu wa kuandaa rasimu na kupigwa kwa kura ya maoni.

Alisema Kamati Kuu pia iliitaka SMZ kuweka bayana kalenda na mchakato wa uundwaji wa Tume huru ya Uchaguzi na kutaka maelezo ya kina kuhusu uundwaji wa kamati ya uteuzi ya wajumbe wa Tume za Uchaguzi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) wakiwamo mwenyekiti, makamu mwenyekiti, mkurugenzi na upatikanaji wa wajumbe wake.

“Kamati Kuu imeazimia kumtaka Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kufanya uamuzi juu ya masuala yaliyoachwa kwenye kikosi kazi cha Zanzibar baada ya mashauriano na Makamu wa Kwanza wa Rais wa SMZ kuhusu kura ya mapema na mfumo wa kupatikana kwa kamati ya uteuzi wa wajumbe wa ZEC.

Kuhusu Mwelekeo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar (SUK), Shaibu alisema Kamati Kuu ilielekeza uamuzi kuhusu suala hilo uwasilishwe kwa barua rasmi kwa Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Rais Mwinyi na kunakiliwa kwa barua hiyo kwa Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan.

Kamati hiyo pia imeazimia kuwaagiza viongozi wakuu wa chama hicho kuonana na mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao nchini na serikali zao ili kuwaeleza mwenendo wa sasa aliodai usioridhisha wa SUK.

Shaibu alisema chama chao kinamtaka Rais Mwinyi kuweka wazi ripoti ya kikosi kazi alichokiunda kushughulikia masuala ya demokrasia Zanzibar kama ambavyo imefanyika kwa Rais wa Tanzania.

“Penye nia ya dhati, masuala yanayogusa maslahi ya umma huwekwa wazi, hakuna sababu inayohalalisha kufichwa kwa ripoti ya kikosi kazi.

“Kwa kuwa kwenye vikao mbalimbali Rais wa Zanzibar amekuwa akieleza kuwa hoja za maridhiano zitatekelezwa kwa ufanisi, atakapochaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM, Kamati Kuu imeweka muda wa utekelezwaji wa makubaliano baina ya Rais Mwinyi na marehemu Maalim Seif Sharif Hamad waliyoyafanya kabla ya ACT-Wazalendo kuingia kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tunataka utekelezaji kwa vitendo wa hoja tatu zilizowasilishwa kwa Rais Mwinyi.

“Mbali na hoja ya kuachiwa huru viongozi wa ACT-Wazalendo waliokuwa mahabusu au wameshikiliwa kwa njia nyingine ambayo imetekelezwa, Kamati Kuu inataka utekelezwaji wa hoja ya kufanyika uchunguzi huru wa kimahakama kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, kuwapatia fidia waathirika wa uchaguzi huo na kufanyiwa mapitio na mabadiliko mfumo wa uchaguzi na Mahakama wa Zanzibar,” Shaibu alisema.

# Kina cha maji Bwawa la Nyerere chafikia mita 116

**Na Mwandishi Wetu**

KINA cha maji kwenye bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere (JNHPP) kimefikia mita za uzajo 116 kutoka usawa wa bahari, ikiwa ni mwezi mmoja tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipofunga rasmi lango la kuchepusha maji na kuruhusu yajae bwawani.

Mwishoni mwa wiki, Mhandisi Mkazi, Emmanuel Mwandambo kutoka Kampuni ya TANROADS Engineering Consulting Units (TECU), alibainisha hayo alipotoa ufafanuzi wa mambo mbalimbali kwa makatibu wakuu wastaafu waliotembelea mradi huo.

Viongozi hao ni makatibu wakuu na manaibu katibu wakuu wastaafu waliowahi kuhudumu katika Wizara ya Nishati kwa nyakati tofauti wakiongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu Mkuu wa Baraza la Mawaziri ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Zena Ahmed Said.

Desemba 22, mwaka jana, Rais Samia alifunga lango la kuchepusha maji na kuruhusu maji kuanza kujaa kwenye bwawa kwa kuwa wataalamu wameeleza ili pajae panahitaji misimu miwili kamilifu na matarajiao ni kuanza kuzalisha umeme mwakani.

Akizungumza baada ya kutembelea maeneo mbalimbali ya mradi huo, Zena alisema mradi huo ni mkubwa na unaendelea vizuri na kwamba taarifa waliyopewa ujenzi umefikiwa asilimia 80.22 na inategemewa hadi kufikia Januari 2024, umeme wa kwanza utaanza kuzalishwa.

Alisema umeme huo utasafirishwa hadi Chalinze ili uungwanishwe kwenye Gridi ya Taifa na kusambazwa kwenda sehemu mbalimbali za nchi yetu.

Kwa mujibu wa Zena, faida mbalimbali za mradi huo unaotarajiwa kuzalisha jumla ya megawati 2,115, ni pamoja na upatikanaji wa umeme wa uhakika ambao utaondoa kabisa changamoto ya upungufu wa umeme.

Pia kupata ujuzi utakaosaidia wengi kwa kuwa vijana wengi walioshiriki katika ujenzi wa mradi huu watabakia na uelewa utakaowawezesha kujiajiri na hata kutumika kwenye miradi mingine inayoendelea.

"Bwawa hili likimalizika kwa kweli litakuwa ni mkombozi mkubwa sana kwa sababu nchi yetu itaweza kupata umeme wa uhakika na kupelekea changamoto ya upungufu wa umeme kubaki historia.

"Kwa hiyo, tuendelee kushirikiana ili tulikamilishe hili na baada ya hapa vijana wetu wengi watakuwa wamepata ujuzi.



Mhandisi Mkazi, Emmanuel Mwandambo, wa Mradi wa Julius Nyerere kutoka Kampuni ya TANROADS Engineering Consulting Units (TECU) akifafanua jambo kwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Zena Ahmed Said pamoja makatibu wakuu wastaafu walipotembelea bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

"Nitoe wito kwa Wizara ya Nishati iweke kanzidata ili kuwatambua wale wote waliohusika kwa sababu nimeambiwa asilimia 90 ya wafanyakazi ni Watanzania," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Felchesi Mramba, alisema mradi huo utakuwa na faida nyingi kwa Watanzania na kwamba serikali imeandaa mipango mingi ya matumizi ya bwawa ambayo ni pamoja na kutenga hekta 400,000 kwenye Rufiji Delta zitakazotumika kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji.

Pia bwawa litatumika kwa ajili ya shughuli za uvuvi na kuwezesha kupatikana kwa maji na umeme wa uhakika pamoja na kuwapatia vijana ajira.

Katibu Mkuu mstaafu, Dk. Avemaria Semakafu, alipongeza serikali na wizara kwa kuendeleza kwa kasi kubwa mradi huo wa kimkakati ambao unategemewa kuwa kichocheo cha maendeleo kwa Watanzania na taifa kwa ujumla. Alitoa wito kwa wizara na TANESCO kuandaa makala maalum itakayowahusisha wadau wote waliohusika katika kuanzishwa kwa mradi huo ili Watanzania waijue historia kamili ya kazi hiyo.

Mradi huo ukikamilika, utazalisha megawati 2,115 ambazo zitaongeza nguvu

katika megawati 1,430 za umeme zinazozalishwa sasa kwenye vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme na kuondoa tatizo la upungufu wa umeme na kuiwezesha nchi kujitosheleza kwa mahitaji ya umeme na kuwa na ziada ya kuuza nchi jirani sambamba na kupunguza gharama za umeme kwa Watanzania.

# RC aagiza msako nyumba kwa nyumba wasioripoti shuleni

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, amewaagiza viongozi na watendaji wote kuanzia ngazi ya mitaa kuwasaka nyumba kwa nyumba watoto wote ambao wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, lakini hadi sasa hawajaripoti shuleni.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Chalamila alisema Mkoa wa Kagera una wanafunzi 59,324 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, lakini waliripoti shuleni hadi Januari 20 ni 35,594 sawa na asilimia 60.

"Ina maana wanafunzi 23,730 ambao ni sawa na asilimia 40 wapo mtaani, viongozi wote kuanzia wakuu wa wilaya kwa kushirikiana na wa halmashauri, tarafa, kata, vijiji na mitaa, fanyeni misako nyumba kwa nyumba mpaka mhakikishe watoto wote hawa ambao hawajaripoti wanapatikana na kuripoti shuleni, ili waanze masomo kabla ya Januari 31, 2023," aliagiza.

Chalamila aliowaonya wazazi watakaobainika kuwatorosha watoto au kushiriki kwa lolote linalosababisha mtoto kutoripoti shuleni, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao ili liwe fundisho kwa wengine wenye nia ya kuzuia watoto kupata haki yao ya elimu.

"Kama unajua wewe mzazi unashiriki kwa njia yoyote kumzuia mtoto asiende shule au unamtumikisha katika shughuli zako za kiuchumi au sababu nyinginezo, serikali haiko tayari kuona mtoto anapotea maana asipopata elimu tunatengeneza kikazi ambacho baadaye tutajutia na ili kuepuka hili ndiyo maana serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia," alisema.

Chalamila alisema kuwa kuanzia sasa, wakuu wa wilaya wanapaswa kupokea taarifa kila siku kutoka kwa wakuu wa shule, zinazoeleza watoto wangapi wameripoti kwa siku husika kwenye shule zilizoko maeneo yao, pia kujua vikwazo vinavyokwamisha wengine wasiripoti ili kutafuta ufumbuzi.

Aliwataka wakuu wa shule kuwapokea watoto wote wanaopelekwa shuleni na wazazi bila kuwawekea vikwazo kwa ambao watakuwa hawajakamilisha vifaa na michango inayotakiwa na kwamba watakaobainika kukwamisha shughuli ya upokeaji wa watoto kwa kuweka misimamo watachukuliwa hatua za kinidhamu.



# Mikutano ACT-Wazalendo kuitikisa mikoa tisa

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA Cha ACT-Wazalendo kimetangaza awamu ya kwanza ya mikutano ya hadhara kwa mikoa tisa ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu (pichani), alisema mikutano hiyo itaanza na mikoa Dar es Salaam, Unguja, Pemba, Tanga, Pwani, Lindi, Tabora, Kigoma na Mkoa wa kichama wa Selous.

Alisema mikutano hiyo inatarajiwa kuanza mwezi ujao kwa Mkoa wa Dar es Salaam Februari 19 na kufuatia na Unguja Februari 26.

Shaibu alisema mikutano hiyo itaendelea Machi 4, 8, 9, 10, 12, 15, 16 hadi 18 huku Pemba ikianza katika tarehe hizo zilizotajwa ikifuatiwa na Tanga, Selous, Tabora na Kigoma zilizopangiwa siku mbili kila moja.

Kwa mujibu wa Shaibu, awamu ya pili ya mikutano



hiyo itatangazwa baadaye.

Alizitaja ajenda zitakazoongoza mikutano ya chama hicho kuwa ni hali ya maisha ya wananchi na mageuzi ya mifumo ya kidemokrasia nchini.

"Kamati Kuu imeelekeza kuwa mbali na ajenda nyinginezo muhimu, mikutano ya hadhara ya chama, itumike kutambulisha ahadi za chama chetu kwa Watanzania na tutachambua changamoto mbalimbali zinazoikabili nchi, namna watawala wameshindwa kuzitatua na kuonyesha sera mbadala za ACT-Wazalendo kutatua changamoto hizo," alisema Shaibu.

Alisema chama hicho kitazindua kaulimbiu yake mpya Februari 18, mwaka huu, wakati Zanzibar itazinduliwa Februari 25.

"Na kaulimbiu hiyo itatambulishwa kwa Tanzania Bara na itatambulishwa rasmi kwa Wazanzibari huko Nungwi Februari 26, mwaka huu," alisema Shaibu.

ACT imetangaza mikutano hiyo baada ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuzindua rasmi mikutano yake juzi, ikianza na mikoa ya Mwanza na Mara.

Hayo yamekuja siku chache baada ya serikali kuruhusu kurejea kwa mikutano ya kisiasa baada ya kuwa imeizuia kwa takriban miaka saba.

# Mwenyekiti wa Kijiji adaiwa kuuza mlima

**Na Idda Mushi,** KILOSA

MWENYEKITI wa Kijiji cha Mamboya wilayani Kilosa mkoani Morogoro, Seif Said, anatuhumiwa kuuza mlima ndani ya hifadhi ya kijiji kwa Sh. milioni moja, ekari tano na nusu za kijiji bila ridhaa ya mkutano mkuu wa kijiji na kuruhusu ukataji miti na uchomaji mkaa.

Kutokana na uamuzi huo, wanakijiji hao wamemkataa hadharani mwenyekiti huyo ambaye anadaiwa kuigawia familia yake maeneo ya vyanzo vya maji huku kukiwa na kasi ya ukataji miti na kuchoma mkaa.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara wa kijiji hicho, Diwani wa Mamboya, Zawadi Amos, alisema vyanzo vingi vya maji kijijini huko vimeharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu kama uchomaji wa mkaa kwa njia ya matanuru kando ya mito na kilimo.

Alidai serikali ya kijiji chini ya uongozi wa Mwenyekiti Said imekuwa ikifanya ubadhirifu wa ardhi kwa kuwauzia wageni mashamba kwa ajili ya kilimo na ufugaji.

"Kila ninapofuatilia ninakosa majibu ya kuridhisha kutoka kwa mwenyekiti, hali hii imesababisha kuendelea kwa migogoro isiyokwisha ya wakulima na wafugaji," alidai diwani huyo.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Alhaj Majid Mwanga, pamoja na uongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilosa, ukiongozwa na Katibu wa chama hicho wilayani hapa, Shaban Mdoe, walifika kijijini huko mwishoni mwa mwiki na kuwatuliza wananchi waliokuwa na hasira dhidi ya mwenyekiti huyo na kuwataka kuwa watulivu wakati serikali ikishughulikia suala hilo.

Viongozi hao walilazimika kutembea kwa miguu umbali wa zaidi ya kilomita 15 kwenda kujionea uharibifu uliofanywa kwenye hifadhi hiyo ya kijiji na kufikia uamuzi wa kumvua madaraka mwenyekiti huyo.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Mwanga, mbali na kumvua uongozi mwenyekiti huyo, alimwagiza Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mamboya kusimamia utaratibu wa kuwaondoa wakulima na wafugaji wote walioko ndani ya hifadhi hiyo ili kulinda vyanzo vya maji visiendelee kuharibiwa.

Mwenyekiti huyo wa kijiji alipohojiwa, alikiri kuhusika na tuhuma hizo ikiwamo utiaji saini na kuuza eneo la kijiji bila ridhaa ya wanakijiji, kuuza mlima na kugawa kiholela maeneo kwa familia yake.




Makatibu Wakuu wastaafu wakiwa kwenye picha ya pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Mhe. Mha. Zena Ahmed Said (aliyekaa katikati mwenye suti ya khaki) akiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhe. Mha. Felchesmi Mramba walipotembelea mradi wa bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere (JNHPP) Jumamosi, tarehe 21 Januari 2023.

TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

# MWITO WA KUTOA MAONI

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mineral Oil Corporation Limited,<br>S.L.P 969,<br>Arusha. | Kiwanja Na. 14, Kitalu "G", Eneo la Viwanda la Themi, Arusha. | Sandesh Kumar Aggawal (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya Vilainishi (Lubricants) |
| 2. | Mnyenye General Supplies Service station<br>S.L.P 154,<br>Karatu – Arusha. | Kiwanja Na. 27/G, Kitalu "G", Eneo la TFA, Karatu, Arusha | Winnie Jublate Mnyenye (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 3. | National Oil Ltd – Tengeru Service station,<br>S.L.P 70048,<br>Dar – es salaam | Kiwanja Na.101/2, Eneo la Tengeru, Arumeru, Arusha | Moteza Augustine Moshi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 4. | Elifuraha Elieza Mbwambo T/A Mau petrol and service station,<br>S.L.P 12465,<br>Arusha. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "J", Eneo la Olasiti, Arusha. | Elifuraha Elieza Mbwambo (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 5. | Mount Meru Petroleum Limited – Meru 9 Petrol Station,<br>S.L.P 7094,<br>Arusha. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "JJ", Mtaa wa RC, Eneo la Kijenge, Arusha. | Atul Mital (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 6. | Kuringe Transport Co.Ltd – Sanya Juu petrol station,<br>S.L.P 50,<br>Siha – Kilimanjaro. | Kiwanja Na. 29, Kitalu "B", Eneo la Sanya juu, Siha, Kilimanjaro. | Liberatus Silvester Temu (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 7. | Mnyone Investment Company Limited,<br>S.L.P 452,<br>Same. | Kiwanja Na. 60, Kitalu "K", Eneo la Same, Kilimanjaro. | Enea Maliki Mnyone (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa gesi ya kupikia (LPG) |
| 8. | Raphael Dominic Mrosso,<br>S.L.P 156,<br>Simanjiro – Manyara. | Kijiji cha Landanai, Simanjiro, Manyara. | Raphael Dominic Mrosso (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 9. | Suma Filling Station,<br>S.L.P 9596,<br>Simanjiro. | Kijiji cha Nyumba ya Mungu, Simanjiro, Manyara. | Athumani Jafari Kitoma (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 10. | GR Oil and Gas Limited,<br>S.L.P 10001,<br>Dar es salaam. | Kiwanjan Na. 71, Kitalu "P",, Kijiji cha Magugu, Babati, Manyara. | Robert Kamanyile (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 11. | Rahabu Logistics Company Limited,<br>S.L.P 12140,<br>Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 3, Kitalu "A", Eneo la Nsonyanga, Mbarali, Mbeya. | Benjamin Freddy Mwandete (Mtanzania | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 12. | Mnyonge Investment Company Limited – Mlowo II,<br>S.L.P 243, Mbozi | Kiwanja Na. 1, Kitalu "C", Mlowo, Mbozi, Songwe. | Daima Jackson Mwashambwa (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 13. | Hossiana Harrison Mbujah - Chapwa,<br>S.L.P 73,<br>Tunduma | Eneo la Msampania, Momba, Songwe. | Hossiana Harrison Mbujah (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa gesi ya kupikia (LPG) |
| 14. | Mzuma Lwitakubi Mganga, S.L.P 232,<br>Ukerewe. | Kijiji cha Chema, Sengerema, Mwanza. | Mzuma Lwitakubi Mganga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 15. | Laurian Burukadi Katarama,<br>S.L.P. 150,<br>Sengerema. | Kiwanja Na. 243, Kitalu "B", Eneo la Mawe matatu, Misungwi, Mwanza | Laurian Burukadi Katarama (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 16. | GBP Tanzania Limited, S.L.P. 1899, Mwanza. | Kiwanja Na. 748 Kitalu "L", Eneo la Pasiansi, Ilemela, Mwanza. | Rashid Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 17. | Lugeye Oil Limited,<br>S.L.P. 11624,<br>Mwanza. | Kiwanja Na. 290, Kitalu "A", Eneo la Wita (Kisesa Trading Centre) Magu, Mwanza. | Boniventura Destery Kiswaga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 18. | Michael Deus Siyantemi, S.L.P 20, Misungwi. | Kijiji cha Mbarika, Misungwi, Mwanza. | Michael Deus Siyantemi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 19. | Sebastian Fransisco Bulunda,<br>S.L.P 44,<br>Buchosa | Kiwanja Na. 2, Kitalu "A", Eneo la Ngoma, Sengerema, Mwanza. | Sebastian Fransisco Bulunda (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 20. | Bugando 1 General Supplies,<br>S.L.P. 442,<br>Geita | Mtaa wa Buhalala -Geita. | Alex Deus Kalimba (Mtanzania) | Leseni ya Kusambaza Gesi ya Kupikia ya LPG |
| 21. | Ongujo Investment Co. Ltd,<br>S.L.P 75,<br>Rorya. | Kijiji cha Ochuna, Rorya, Mara | Ongujo Wakibara Nyamarwa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 22. | ASHICO Tanzania Company Limited, S.L.P.49,<br>Magu | Kiwanja Na. 690 Kitalu "A" Eneo la Sokoni - Lamadi, Busega, Simiyu | Arobogast Olvaris Shirima (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 23. | Saimin Gas Distributors, S.L.P.185, Bukoba | Kiwanja Na. 81, Kitalu "BB" Eneo la Hamugembe, Bukoba, Kagera. | Sabaha Minaz Rajabali (Mtanzania) | Leseni ya Kusambaza Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 24. | Mariam Suleiman Swalimin,<br>S.L.P 386,<br>Bukoba | Mtaa wa Jamhuri Eneo la Miembeni, Bukoba, Kagera. | Mariam Suleiman Swalimin (Mtanzania) | Leseni ya Kusambaza Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 25. | Mama Electrical and General Service,<br>S.L.P. 197,<br>Kibondo. | Mtaa wa Uswailini, Kibondo, Kigoma. | Hija Ahmad Katobagula (Mtanzania) | Leseni ya Kusambaza Gesi ya Kupikia ya LPG |
| 26. | Afroil Investment Limited, S.L.P. 38383,<br>Dar es Salaam | Kiwanja Na. 678, Kitalu "CC", Eneo la Matanda, Shinyanga, Shinyanga. | Hilmy Ahmed Mbarak (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 27. | Gimunta Group Limited, S.L.P. 2161, Shinyanga | Kiwanja Na. 34, Kitalu "Y", Eneo la Ibinzamata, Shinyanga. | Charles Nyangige Matiko (Mtanzania) | Leseni ya Kusambaza Gesi ya Kupikia ya LPG |
| 28. | Hesbon Kataraihya Bukagile,<br>S.L.P 442,<br>Kahama. | Kiwanja Na. 254, Kitalu "T", Eneo la Nyasubi, Kahama, Shinyanga. | Hesbon Kataraihya Bukagile (Mtanzania) | Leseni ya Kusambaza Gesi ya Kupikia ya LPG |
| 29. | Kakusima Alex Kalokola T/A Kagoli Enterprises, S.L.P 617,<br>Kahama. | Mtaa wa Nyahanga, Kahama, Shinyanga. | Kokusima Alex Kalokola (Mtanzania) | Leseni ya Kusambaza Gesi ya Kupikia ya LPG |
| 30. | GBP (T) Ltd – Ipuli Service station<br>S.L.P 3728<br>Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 146 Kitalu "TT" Eneo la Ipuli, Tabora. | Rashid Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 31. | Anwar Saleh Bakhamis T/A Serious Oil Filling Station Mkoka,<br>S.L.P 100,<br>Kibaigwa. | Kijiji cha Mkoka Kibaigwa, Kongwa. | Anwar Saleh Bakhamis (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 32. | Gapco Tanzania Limited – Kitanzini, Iringa,<br>S.L.P 9103,<br>Dar es salaam. | Viwanja Na. 1,2,14 Kitalu "G" Eneo la Kitanzini, Iringa. | Jean-Francois Schoepp (Raia wa Ubelgiji) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 33. | Watende Seleman Msungu T/A Kangesa Service Station,<br>S.L.P 110,<br>Mafinga | Kiwanja Na. 229 Kitalu "A" Boma Mafinga, Iringa. | Watende Seleman Msungu (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 34. | GP 88 - Mapinduzi Petrol Station,<br>S.L.P 3073,<br>Dodoma. | Kiwanja Na. 2 Kitalu "R" Mapinduzi North Iyumbu, Dodoma. | Haleluya Wilfred Kessy (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 35. | Mussa Yohana Mkunda T/A Chikumbi Enterprises,<br>S.L.P 217,<br>Mpwapwa. | Kijiji cha Mbande, kongwa, Dodoma. | Mussa Yohana Mkunda (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 36. | Estim Construction Ltd,<br>S.L.P 19716,<br>Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 181 Western Industrial Area, Dodoma. | Girdharbhai Meghji Ratna Pindolia (Raia wa India) | Leseni ya kituo binafsi ya mafuta |
| 37. | Lake Oil Limited Depot | Kiwanja Na. 46, Kitalu "E", | Ally Edha Awadh | Leseni ya jumla ya |
| | Kigamboni Dar Es Salaam,<br>S.L.P. 5055,<br>Dar es Salaam. | Eneo la Kigamboni, Dar es salaam. | (Mtanzania) | Mafuta |
| 38. | Silafrica Tanzania Limited<br>S.L.P. 11078,<br>Dar es salaam. | Kiwanja Na. 30, Kitalu "B", Eneo la Chang'ombe, Temeke, Dar es Salaam. | Alpeshkumar Jayantilal Patel (Raia wa India) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa matumizi binafsi |
| 39. | Lake Oil Limited Nane Nane Morogoro,<br>S.L.P. 5055,<br>Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 228/5, Kitalu"A", Eneo la Mlima Kola, Morogoro. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 40. | Lake Oil Tandika Dar es Salaam,<br>S.L.P. 5055,<br>Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 51 na 80, Kitalu "L", Eneo la Temeke, Temeke, Dar es salaam. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 41. | Rashal Petroleum Limited Mlimba,<br>S.L.P 198,<br>Mlimba. | Kiwanja Na. 17, Eneo la Gezailole, Kilombero, Morogoro. | Farhiya Hersi Warsame (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 42. | Mek One Industries<br>Ifakara Filling Station<br>S.L.P. 5055,<br>Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 320, 322 na 324, Kitalu "C", Eneo la Ifakara, Kilombero, Morogoro. | Mohamed Eidha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 43. | Mkuti Service Station Ltd- Masasi,<br>S.L.P. 10,<br>Masasi. | Kiwanja Na. 10, Kitalu "C/A", Eneo la Masasi Mtwara. | Abdulaziz Wallimohamed Abdulrehman (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 44. | Afroil Investment Limited.<br>S.L.P. 38383,<br>Mtwara. | Kiwanja Na. 233, Kitalu "F", Eneo la Magomeni, Mtwara. | Hilmy Ahmed Mbarak (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 45. | Delta Corp Tanzania Ltd,<br>S.L.P. 7387,<br>Pwani. | Kiwanja Na. 14, Eneo la Dundani, Mkuranga, Pwani. | Manan Goel (Raia wa India) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

217238302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mashabiki Simba msimvimbishe Chama, kocha anajua zaidi

**KUMEKUWA** na mjadala mkubwa kutoka kwa mashabiki wa soka nchini husussan wa Simba wakipinga na kumwona Kocha Mkuu mpya wa klabu hiyo, Robertinho Oliveira, hafai baada ya kufanya mabadiliko 'sub' na kumtoa Clatous Chama.

Robertinho ambaye katika mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Bara akiwa na Simba Jumatano iliyopita, aliiongoza kushinda mabao 3-2 dhidi ya Mbeya City, alimtoa Chama dakika ya 31 ya kipindi cha kwanza na kumwingiza Pape Sakho.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Chama alitolewa wakati huo matokeo yakiwa bao 1-1, huku akiwa mpishi wa bao hilo, jambo ambalo mashabiki wa Simba walizomea uamuzi huo uwanjani hapo. Malalamiko hayo yaliendelea hata kwa mashabiki waliokuwa wakifuatilia mechi hiyo kupitia televisheni na kisha mjadala mkubwa kutawala vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Wengi wakidai haiwezekani Chama kutolewa kwa kuwa yeye ndiye mhimili wa timu na amekuwa akiibeba kutokana na maamuzi yake sahihi ambayo amekuwa akiyafanya uwanjani. Mashabiki hao wamefika mbali huku baadhi wakitaka atimuliwe.

Hata hivyo, mabadiliko aliyoyafanya Robertinho yalijibu baada ya muda mfupi tu kwani Simba ilipata bao la pili kwa mkwaju wa penalti iliyofungwa na Saido Ntibazonkiza kabla ya Sakho aliyechukua nafasi ya Chama kufunga la tatu.

Bao hilo la Sakho lilimuinua Robertinho aliyewageukia mashabiki uwanjani hapo na kushangilia kwa furaha kubwa, ikiwa ni ishara ya kuwaonyesha kwamba yeye ni kocha mwenye taaluma hiyo, hivyo hakufanya makosa kumtoa Chama.

Kwa ujumla mashabiki wa Simba wanapaswa kuelewa jambo moja kwamba kocha anapaswa kuachwa huru kuamua ni mchezaji gani wa kuanza, kutokea benchi na yupi anayestahiki kufanyiwa mabadiliko wakati wowote.

Kitaalamu kocha anapokuwa nje na wasaidizi wake ana akili ya kuusoma mchezo mzima na anapofanya mabadiliko anakuwa tayari ameona tatizo liliko katika kikosi chake na udhaifu wa wapinzani, hivyo kutoa maelekezo ya nini cha kufanya kwa mchezaji anayeingia. Kadhalika, Chama si mchezaji mkubwa pekee anayeibeba timu yake katika ulimwengu wa soka, ambaye ameanza kufanyiwa mabadiliko, tumeshuhudia kwa nyakati tofauti Lionel Messi na Cristiano Ronaldo 'CR7' wakiwa kwenye ubora wao wakifanyiwa mabadiliko na timu zao kupata matokeo chanya kama iliyotokea kwa Simba katika mchezo huo.


Lakini ni mashabiki hao hao wa Simba ambao hivi karibuni kabla ya dirisha dogo la usajili kufunguliwa na kufungwa Januari 15, mwaka huu, walikuwa wakilalamika na kuutaka uongozi usajili kiungo mshambuliaji mwenye uwezo kama Chama ama zaidi yake.

Hiyo ilitokana na timu hiyo kuwa katika wakati mgumu wa kupata matokeo pindi Chama alipokuwa nje akitumikia adhabu ya kufungiwa michezo mitatu, hivyo uongozi uliliona hilo na kumsajili Ntibazonkiza.

Hivyo, alichokifanya Robertinho katika mchezo huo, sisi tunamwelewa kwani mbali na sababu nyingine zilizotolewa, ni wazi uamuzi wa kumtoa Chama alitaka pia kuona ni namna gani Ntibazonkiza anaweza kuibeba timu mabegani mwake pindi Chama akiwa hayupo.

Kwa mantiki hiyo mashabiki wa Simba na wapenzi wa soka kwa ujumla hawana budi kuheshimu taaluma za makocha wao, lakini kutambua Robertinho bado anaendelea kuwasoma na kujaribu kutambua uwezo wa kila mchezaji kulingana na mfumo wake, hivyo kuendelea kusema Chama hapaswi kutolewa hata kama akikosea ni kumvimbisha na kumfanya ashindwe kuheshimu maamuzi ya kocha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Makubaliano wachezaji wa mkopo yaheshimiwe

**BAADA** ya dirisha dogo la usajili kumalizika na kuona wachezaji mbalimbali wakisajiliwa kutoka ndani na nje ya nchi, pia tumeshuhudia baadhi wakitolewa kwa mkopo.

Baadhi ya wachezaji wametoka kwenye klabu moja kwenda nyingine. Kama inavyoeleweka kwa wanasoka kuwa mara nyingi wachezaji wanaotolewa kwa mkopo ni wale ambao wameshindwa kuingia kwenye kikosi cha kwanza na cha akiba, hivyo hutolewa kwenye klabu nyingine ili wapate muda mwingi wa kucheza.

Wengine wanakuwa wameshuka viwango, hivyo wanapelekwa kwenye klabu zingine za madaraja ya kati ambazo timu zao hazina presha sana ili kurudisha viwango na kujiamini.

Wakati mwingine kuna wachezaji wana uwezo mkubwa na vipaji, lakini kwa sababu hawana majina na uzoefu wanapelekwa kwenye klabu zingine kwa ajili ya kucheza na kuthibitisha uwezo walionao, na kisha baadaye kurejeshwa tena kwenye klabu mama.

Hapa nchini, kuna wakati wachezaji wa mkopo wanakwenda 'kukiwasha' huko wanakokwenda kiasi cha klabu zao zinazowamiliki kuwarejesha tena, lakini hata hivyo wengine wakishaondoka basi hadi mikataba yao inamalizikia huko huko na wanakuwa huru, sasa inakuwa ni hiari yao kuingia mkataba na timu walikopelekwa kwa mkopo au nyingine.

Tumeona kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baadhi ya wachezaji wakipelekwa kwa mkopo sehemu mbalimbali kwa makubaliano kati ya klabu na klabu.

Hata hivyo, kumekuwa na mijadala inayoendelea kwenye majukwaa mbalimbali ya michezo kuwa wachezaji hao waachwe wacheze wanapokutana na timu zao mama.

Yaani mchezaji wa Azam FC aliyepelekwa Dodoma Jiji kwa mkopo, zitakapokutana timu hizo basi acheze tu na kusiwe na vipingamizi.

Ni kweli inawezekana kama klabu iliyomtoa haioni tatizo lolote lile, lakini isiwe nongwa kama ikikataa asicheze kwa sababu klabu mama nayo ina haki ya kufanya hivyo. Kanuni hizo zimechukuliwa kutoka Ulaya na hata walioweka hivyo walikuwa na sababu zao nzuri tu na muhimu, hivyo ziheshimiwe.

Mijadala imekuwa ikidai kuwa kitendo cha klabu mama kutomruhusu mchezaji kucheza dhidi ya timu yake iliyomtoa kwa mkopo ni kutomtendea haki mchezaji na pia klabu iliyomchukua.

Kama nilivyosema hapo juu, huu uwe ni mtazamo wa klabu yenyewe na si kuilazimisha. Ikiona acheze basi hakuna tatizo, lakini ikiona izuie na klabu iliyomchukua kukubaliana na hilo, basi makubaliano yaheshimiwe.

Nionavyo mimi ni kwamba mchezaji anayecheza kwa mkopo akicheza na kuifunga au kusababisha timu yake mama kupoteza mechi, au kutolewa kwenye michuano au kombe husika, anaweza kuwa adui kwa mashabiki na hata kama akitaka kurejea, wapenzi na mashabiki wanaweza kucharuka na kukataa.

Wengi wanaangalia upande mmoja tu kuwa mchezaji anatakiwa kuithibitishia timu yake mama kuwa ana uwezo kwa kuikamia na kucheza vizuri siku ya mechi hiyo, bila kuangalia upande wa pili kuwa anajiweka kwenye mazingira magumu pia mbele ya mashabiki.

Halafu pia kwa soka la Tanzania kuna mambo mengine ya nje ya uwanja, inawezekana kabisa mchezaji anayechezea timu kwa mkopo, akacheza chini ya kiwango dhidi ya timu yake mama kwa sababu bado ni mali yao na pia wanaendelea kumlipa mshahara. Hata kama makubaliano ya mshahara ni kila klabu kulipa nusu, lakini mkataba bado upo kwenye klabu yake ya awali.

Kwa maana hiyo, kwa maoni yangu binafsi naona kipengele cha mchezaji wa mkopo kutocheza kwenye mechi dhidi ya timu yake iliyomtoa kina afya zaidi kuliko kumruhusu kucheza.

Kinamwepusha mchezaji huyo na mengi, mbele ya mashabiki kama akisababisha timu yake mama kufungwa, lakini kutuhumiwa kucheza chini kiwango kama timu yake ya mkopo pia ikipoteza.

Kikubwa zaidi hapa ni kwamba tuziache klabu zenyewe zinazopeana mchezaji kuangalia ni vipengele gani ambavyo wanakubaliana na viheshimiwe kwa maslahi ya pande zote tatu.

# Mbaroni tuhuma kuiba mtoto

**Na Rose Jacob,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limemkamta Mariam Julius (23) kwa tuhuma za kuiba mtoto mwenye umri wa siku moja.

Akizungumzia tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Wilbroad Mutafungwa, alisema walimkamta Mariam baada ya kufanya msako wa kuwatafuta watuhumiwa wa wizi wa watoto wawili walioripotiwa kuibwa wilaya za Ilemela na Sengerema mkoani hapo.

"Mnamo Januari 10 mwaka huu, majira ya 13:30 mchana, mtoto wa kiume mwenye umri wa siku moja, mkazi wa Mtaa wa National Magharibi wilayani Ilemela mkoani Mwanza, aliibwa na mwanamke asiyejulikana," Kamanda Mutafungwa alisimulia.

Alisema kuwa Januari 9, mwaka huu, mama wa mtoto huyo alijifungua kwenye Kituo cha Afya Buzuruga na kuruhusiwa kutoka kituoni siku iliyofuata.

Alidai kuwa alipotoka na kufika nje ya kituo hicho, alikutana na Mariam ambaye alimwomba waende naye nyumbani akapumzike.

"Mama wa mtoto huyo alikubali, baada ya kufika nyumbani ambako Mariam alimpeleka, alimpelekea maji bafuni mzazi ili akaoge, wakati akiendelea kuoga, ndipo mwizi huyo alitoroka na mtoto kwenda naye mahali kusikojulikana," alisimulia Kamanda Mutafungwa.

Alisema kuwa kufuatia tukio hilo, polisi walitoa taarifa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari, hivyo kufanikiwa kumkamata mwanamke huyo akiwa na mtoto huyo ambaye hakudhurika.

Kamanda Mutafungwa alisema walimkamata Mariam Januari 18, mwaka huu, akiwa nyumbani kwake alikopanga maeneo ya Nyakato Mashariki wilayani Ilemela. Alisema kuwa kilichosaidia kufichua uovu huo ni mtoto huyo kulia muda wote, hivyo taarifa ziliwafikia polisi na walipofika wakiwa na mama wa mtoto huyo Joyce Mbuya (23), alimtambua mwanawe.

"Baada ya mahojiano, mtuhumiwa alikiri kutenda kosa hilo kwamba alimwiba mtoto huyo kwa sababu anampenda sana mume wake na alikuwa akimuuliza kuhusu kupata mtoto, hivyo aliamua kutumia njia ya kumhadaa mumewe kuwa ni mjamzito," alisema Kamanda Mutafungwa.

Alisema Jeshi la Polisi pia lilimhoji Mongella Laban ambaye ni mume wa Mariam kuhusu tuhuma za wizi wa mtoto, likimbana kwa kutokutoa taarifa baada ya kumwona mkewe ana mtoto mchanga ilhali alijua hakuwa mjauzito.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete (wa pili kulia), akimsikiliza mwakilishi wa kampuni ya TotalEnergies alipotembelea mabanda ya maonyesho kwenye mkutano mkuu wa 7 wa Chama cha Wamiliki wa Malori nchini (TATOA). Kushoto ni Mwenyekiti wa chama hicho, Elias Lukumay. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baadhi madaktari watuhumiwa kulewa wakiwa kazini

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

WANANCHI wanaokwenda kupata huduma za matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida, wamedai baadhi ya madaktari wanakwenda kazini wakiwa wamelewa na kushindwa kuhudumia wagonjwa.

Walimlalamikia Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, kwenye kikao cha kusikiliza kero wilayani Manyoni.

"Januari 4, mwaka huu saa 3:00 usiku nilimpeleka mtoto wangu katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni ambaye alikuwa ameumia kidole, nikamkuta daktari mmoja ambaye alikuwa amelewa chakali na kushindwa kumhudumia kabisa mgonjwa kwani alikuwa hajiwezi," alidai Prisca Maleta.

Alidai katika hali ya kushangaza, daktari huyo mlevi aliwaambia kama wapo jirani wachukue vifaa vya matibabu wakavifanyie usafi na kisha wamsafishe jeraha (kidonda) mgonjwa na kumwekea dawa.

Maleta alisema baada ya kuambiwa hivyo na daktari huyo alilazimika kumchukua mtoto wake saa nane usiku na kumpeleka katika hospitali binafsi eneo la sokoni Manyoni ambako alipatiwa huduma ya kwanza.

Maleta, alisema siku iliyofuata alimpeleka mtoto wake kupata matibabu katika Hospitali ya St. Gasper inayomilikiwa na Kanisa Katoliki iliyoko Halmashauri ya Itigi.

Alimwomba Mkuu wa Mkoa Singida, Serukamba awasaidiwe kuondolewa kero hizo kwa sababu wananchi wengi wanaathiriwa na hali hiyo katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni kutokana na matukio ya baadhi ya madaktari kwenda kazini wakiwa wamelewa yamekuwa yakijitokeza mara nyingi.


Kutokana na kero hiyo, Serukamba, aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani Manyoni, kuchunguza utendaji wa watumishi wakiwamo madaktari katika hospitali hiyo na apelekewe taarifa ya uchunguzi huo Ijumaa, wiki hii.

Alisema utaratibu huo wa kukutana na wananchi, kusikiliza kero zao na kuzipatia utatuzi papo hapo ni endelevu na atakutana na wananchi katika kila wilaya mara moja kwa mwezi.

Malalamiko yaliyotawala ni migogoro ya ardhi na uamuzi ulifikiwa kwamba Kamishna wa Ardhi Msaidizi wa Mkoa Singida, Shamim Hoza, ashirikiane na watumishi wa ardhi wa wilaya hiyo kupitia migogoro yote ya viwanja na watoe mapendekezo kuhusu njia zinazoweza kuimaliza zikiwamo za maridhiano.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Manyoni, Fadhili Chimsala, aliagizwa kushirikiana na watendaji wake kuorodhesha migogoro yote ya umiliki wa mashamba na usafishaji wake, waite kila muhusika na kuzungumza nao mpaka wafikie maafikiano, yaandikwe na kutiwa saini na pande zote husika.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed





Moja ya magari ya Kampuni ya Mighty Logistic likishusha shehena ya makaa ya mawe kwenye Bandari ya Mtwara tani 55,000 kutoka Kampuni ya Jitegemee Holding CCM ya mkoani Ruvuma yakisafirishwa nchi za Ubelgiji, Ufaransa na Hispania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima Mbarali wamlilia Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu,** Mbarali

WAKULIMA wa maeneo ya Mnazi, Mwanavara na Madibira wilayani Mbarali mkoani Mbeya, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuingilia kati marufuku ya kuendelea na kilimo katika maeneo hayo, baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kutatua mgogoro katika Bonde la Usangu uliodumu kwa miaka 15.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi kwa nyakati tofauti, walisema wanashangaa marufuku hiyo wakati Januari 16, 2023 mkoani Mbeya, Waziri Mkuu Majaliwa alisema serikali imefanya maboresho makubwa kwenye Tangazo la Serikali Namba 28, ambayo itawawezesha wananchi wote kufanya shughuli za kilimo na ufugaji endelevu.

"Hatujasikia Waziri Mkuu akipiga marufuku wakulima wa maeneo hayo wasiendelee na kilimo bali tulisikia akisema wakulima wote waendelee na kilimo na kauli hiyo aliitoa katika kikao na wadau waliowekeza katika Bonde la Usangu, sasa Juma Homera ametoa wapi hilo agizo amepewa na nani kama waziri mkuu karuhusu, yeye ni nani kutuzuia tusifanye kilimo?" Alihoji Mwakibolwa Mwakalenga.

Alisema kuwa Waziri Mkuu alisema marekebisho ya tangazo hilo yatawezesha pia baadhi ya vitongoji vilivyokuwa vimetangazwa awali kuwa ndani ya hifadhi, kuachwa nje ya mipaka ikiwamo kutoa eneo la hekta 74,000 kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji.

Alimnukuu Waziri Mkuu kwa kusema kuwa, "Hii GN 28, serikali tumeamua kuitafutia ufumbuzi baada ya vikao vingi na wadau kwa faraja kabisa, nataka niwaambie tumefikia hatua nzuri itakayowezesha kila anayejishughulisha na kilimo kuendelea na kilimo chake na kila anayejishughulisha na mifugo kuendelea na ufugaji wake."

Kwa upande wake Amos Mgimbaji, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali wanajua fika kuwa katika maeneo hayo ambayo mkuu wa mkoa kapiga marufuku wakulima kuendelea na kilimo kuna Chama cha Ushirika cha Nguvu Kazi, ambacho nacho kimekopa fedha nyingi kutoka Benki ya CRDB kwa ajili ya kuendesha kilimo.

"Mnazi, Mwanavara na Madibira tuna chama cha ushirika cha wakulima wa mpunga na kwa kupitia chama hicho tumekopa fedha nyingi kwa ajili ya kilimo, sasa tunavyoambiwa tusifanye kilimo wala kuonekana katika maeneo hayo fedha hizo zitarudishwaje au serikali ya mkoa inataka tufilisiwe? Maana Waziri Mkuu ameruhusu, lakini Juma Homera amegoma tutafika kweli?" Alihoji Mgimbaji.

"Unajua viongozi hawa wa mkoa kwa kujua ama kwa kutokujua wanatoa kauli kama hizi za kutuumiza sisi, wanashindwa kujua tumekopa fedha nyingi katika benki ili tufanye kilimo na baadaye tuzirejeshe kwa zuio hili la mkuu wa mkoa tutaweza kurejesha marejesho kweli?"

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Homera, alisema katika maeneo ya Mnazi, Mwanavara na Madibira, hayaruhusiwi kufanya shughuli za kilimo kwa kuwa hilo lipo ndani ya hifadhi na ni bakuli la kukusanyia maji ya kuingia katika Mto Ruaha Mkuu.

Alisema eneo hilo lipo ndani ya mita 20 kutoka Mto Ruaha Mkuu na amewaomba wakulima hao kuwa watulivu kwa kuwa serikali ya mkoa inawatafutia eneo kubwa kwa ajili ya kuendelea na kilimo chao kama kawaida na kuwataka wasiwe na wasiwasi.

"Mimi nawaomba wananchi hawa wasiwe na wasiwasi kwani nitahakikisha wanapata eneo bora na lenye miundombinu yote ya kufanya shughuli za kilimo cha kisasa na chenye tija," alisema Homera.

# Mashahidi 10 kutoa ushahidi uhamishaji umiliki wa magari

**Na Kulwa Mzee**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya kutoa taarifa za uongo mahakamani kuhamisha umiliki wa magari 14 na kujipatia fedha kwa udanganyifu inayomkabili Shabani Cosla na dalali wa mahakama, unatarajia kuita mashahidi 10 na vielelezo 12 kuthibitisha ulaghai.

Wakili wa Serikali, Magreth Kisoka, alidai hayo mwishoni mwa wiki katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala mbele ya Hakimu Mfawidhi, Suzan Kihawa, baada ya kumaliza kuwasomea washtakiwa hoja za awali.

Alidai washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 31 yakiwamo ya kutoa taarifa za uongo 27, kujipatia mali kwa njia ya udanganyifu, makosa matatu na moja la kujipatia fedha kwa ulaghai.

Wakili alidai katika jumla ya mashtaka hayo mshtakiwa Cosla anakabiliwa na mashtaka 23 ya kutoa taarifa za uongo. Inadaiwa Machi 23, mwaka 2012 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, alitoa taarifa za uongo katika mahakama hiyo kwa kuwasilisha shauri la madai namba 99 la mwaka 2012 akionyesha Kampuni ya Escon Borewall Limited ilisajiliwa Tanzania wakati sio kweli.

Katika mashtaka mengine mshtakiwa wa kwanza anadaiwa kati ya mwaka 2012 na 2020 alitoa taarifa za uongo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwa ni mmiliki halali wa gari namba T844 AKV aina ya Fuso Truck wakati si kweli.

Mshtakiwa huyo anadai kutoa taarifa za uongo katika mahakama hiyo akionesha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imehamisha umiliki wa magari 14 kutoka kwa Kampuni ya Escon Borewell kwenda kwa Kampuni ya SBJ Borewells na Target Borewells Limited wakati akijua si kweli.

Katika mashtaka ya kutoa taarifa za uongo yanayomkabili mshtakiwa wa pili ambaye ni dalali wa mahakama, Charles Sengo, inadaiwa alionyesha Mariyam Hamadi kanunua magari manne katika mnada kwa jumla ya Sh. 275,000,000 wakati si kweli.

Wakili alidai katika shtaka la 28 la ulaghai, mshtakiwa wa kwanza alijipatia gari lenye namba za usajili T975 BQM aina ya Ashok Leyland lenye thamani ya Sh. milioni 75. Inadaiwa katika shtaka la 29 na 30 mshtakiwa huyo alijipatia magari mengine mawili yenye namba za usajili T346 CHC lenye thamani ya Sh. 65,000,000 na T344 CHC lenye thamani ya Sh. 60,000,000, yote aina ya Ashok Leyland akionesha yaliuzwa katika mnada wa hadhara kutokana na amri ya mahakama katika shauri namba 99 la mwaka 2015 wakati si kweli.

Shtaka la mwisho anadaiwa Aprili 11, 2019 akiwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Fahak kwa ulaghai alijipatia Sh. milioni 185 kutoka katika akaunti ya mahakama iliyoko Benki Kuu namba 99212697226 kwenda kwenye akaunti ya kampuni yake namba 0150515062000 akionyesha fedha hizo zilipatikana katika mnada uliofanyika Septemba 11, 2016 wakati si kweli.

Washtakiwa katika maelezo yote walikubali taarifa zao binafsi na kukana maelezo yote ya makosa yao, kesi imepangwa kuanza kusikilizwa Februari 23, mwaka huu.

# Watoto chini umri miaka 15 wahusishwa wizi, ubakaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

WATOTO wenye umri chini ya miaka 15 katika Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida wanadaiwa kushiriki vitendo vya wizi na ubakaji nyakati za usiku na kuzua taharuki.

Malalamiko hayo yaliibuliwa na wananchi wa Kijiji cha Puma, wilayani humo katika mkutano wa hadhara ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba ya kusikiliza kero mbalimbali na kuzipatia ufumbuzi.

Mmoja wa wananchi mkazi wa kijiji hicho, Joramu Zakaria, alisema vitendo vya uhalifu vimekithiri katika eneo hilo kwa kiwango cha mtu kutokuwa na uhakika wa kuamka salama.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Samwel Mdimu, alisema walifanya msako na kukamata baadhi ya watoto hao na wazazi wao walikiri hawana pa kuwapeleka.

Samwel alimweleza Mkuu wa Mkoa kwamba walipowakamata na kuwafikisha Kituo cha Polisi, Maofisa wa Polisi walishauri waachiwe kwa kuwa walikuwa na umri mdogo na kuwataka wazazi wao waelezwe ili wawaonye.

Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Ikungi, Suzana Kidiku, aliahidi kulishughulikia suala hilo kwa kuwashirikisha maofisa wa ustawi wa jamii, viongozi wa kijiji na kuwa wanatarajia kufanya msako wa kuwabaini wahalifu zaidi.

Serukamba aliviagiza vyombo vya ulinzi na usalama wilayani Ikungi kufanya msako wa kina na kuwabaini watoto wenye umri chini ya miaka 15 wanaotajwa kushiriki vitendo vya wizi na ukabaji na kuwafungulia mashtaka.

Aidha, Serukamba alikemea tabia ya baadhi ya watu wanaoshiriki kuiba miundombinu ya barabara na umeme ambayo imesemekana inatumika kutengenezea mikokoteni na majembe ya kukokotwa na wanyama.



## Ekari 500 za alizeti, ngano zaharibiwa na wanyamapori

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

EKARI zaidi ya 500 zilizokuwa zimepandwa mazao ya alizeti na ngano zimeharibiwa na wanyamapori katika Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro na kusababisha hasara kubwa ya kiuchumi kwa wakulima.

Kutokana na uharibifu huo, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Mazao Mchanganyiko cha Wilaya hiyo, Felix Mosha, amemwomba Mkuu wa Wilaya ya Siha, Thomas Apson, kuagiza maofisa wanyamapori na idara ya maliasili, kuwadhibiti wanyamapori wanaoingia katika mashamba ya wakulima pamoja na kuyadhibiti makundi ya mifugo yanayotoka wilaya jirani.

Mosha, alizungumza juzi mbele ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Apson, ambaye alishiriki mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika wilayani humo, ambao pamoja na mambo mengine ulijadili uvamizi wa wanyama hao na athari zake kiuchumi.

"Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, tunakuomba uchukue hatua za kudumu za kuwadhibiti wanyamapori na mifugo ya jamii ya wafugaji wa Kimasai, inayofanya uharibifu mkubwa wa mazao na kuwasababishia wakulima wetu hasara ya mabilioni ya fedha kila mwaka.

"Mimi binafsi nimeathirika zaidi na wanyamapori na mifugo ya wafugaji, ambao kwa mwaka mzima wamehamia kwenye shamba langu. Kwa mwaka jana na mwaka huu nimeshindwa kulima kutokana na hofu ya wanyama hao pamoja na uvamizi wa mifugo ya wafugaji wa jamii ya Kimasai."

Wanyamapori tishio ambao wamekuwa wakivamia na kuharibu mazao ya wakulima wilayani humo ni tembo, twiga, nyumbu, pundamilia na swala.

Katika mkutano huo, baadhi ya wakulima, akiwamo Petro Munyuki, alisema wanyamapori na mifugo hiyo ya wafugaji wa Kimasai, imekuwa janga kubwa kwa wakulima huku wakikosa fidia yoyote ya mazao yao na hivyo kujikuta wakibaki masikini, licha ya kufanya kilimo hicho kwa kutumia mikopo ya taasisi za fedha.

"Mazao mengi yaliyoharibiwa ni ngano, shairi, maharage, alizeti, njegere, viazi na karoti. Lakini baadhi ya wakulima wamekuwa wakijeruhiwa kwa kupigwa fimbo na wafugaji, ambao inadaiwa wengi wao wanatoka wilaya jirani pamoja na nchi jirani,"alisema.

Mkulima mwingine, Manase Ntaganda, aliiomba serikali ifikirie kuanza kukikodishia kwa muda mrefu ushirika huo mashamba makubwa manne ambayo ni mali ya Shirika la Taifa la Kilimo na Chakula (NAFCO), ambayo kwa sasa hayatumiki ili walime mazao ya ngano, shayiri, maharage, njegere, karoti na viazi.

Akijibu ombi hilo la wakulima, Mkuu huyo wa Wilaya, alieleza hatua zilizochukuliwa tayari na serikali ni pamoja na kuunda kikosi kazi cha vyombo vya ulinzi na usalama cha kuwadhibiti wanyama na mifugo. "Kutokana na malalamiko haya naagiza serikali za vijiji kuja na sheria ndogo zenye makali ya faini isiyopungua Sh. 500,000 kwa kila mfugo utakaokamatwa kwenye mashamba ya wakulima. Naamini wakitekeleza hili, adhabu hii itasaidia pia kudhibiti uingizaji wa mifugo kwenye shamba la miti la serikali," alisema.

# Akamatwa akitafuta mteja wa kununua meno ya tembo

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKAZI wa Wilaya ya Babati, mkoani Manyara (jina limehifadhiwa) anashikiliwa na Jeshi la Polisi baada ya kukutwa mtaani akitafuta mteja wa kununua meno ya tembo wanaosadikiwa kuuawa katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Mtuhumiwa huyo alikamatwa juzi katika Kijiji cha Matufa na askari wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, akiwa na meno matatu ya tembo yenye uzito wa kilogramu 33.5 yakiwa na thamani ya Sh. milioni nane.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi, George Katabazi, mtuhumiwa huyo mwenye umri wa miaka 33 anaendelea kuhojiwa na makachero wa polisi ili kubaini mtandao huo wa ujangili na biashara ya nyara za serikali.

"Huyu mtuhumiwa ambaye tunaendelea kumhoji, alikamatwa na askari wa NCAA kwenye hicho kijiji akiwa anatafuta wateja wa kuwauzia meno hayo ya tembo. Tukikamilisha upelelezi wetu tutamfikisha mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili,"alisema.

Aidha, Kamanda Katabazi alisema katika tukio lingine, askari wanyamapori kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wamewakamata watu wengine wawili, wakazi wa Wilaya ya Simanjiro, wakiwa na nyamapori za wanyama mbalimbali, wakiwamo digidigi bila ya kuwa na vibali vya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori nchini (TAWA).

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa Januari 18, mwaka huu, majira ya saa 2:00 usiku katika Mtaa wa Jitegemee, Wilaya ya Simanjiro.

Alisema nyama hizo zilikuwa zikisafirishwa kwa pikipiki, ambayo hakuitaja namba zake za usajili, lakini akataja nyama hiyo ina thamani ya Sh. milioni nane.



Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange (wa pili kulia), akikabidhi cheti cha ushindi wa utekelezaji wa mkataba wa lishe kwa kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka jana kwa Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu mkoani Manyara, Adam Mhako. Kulia ni Mganga Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Dk. Damas Kayera. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# NHC yaja na mbinu mpya kuinusuru miradi yake

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), limekuja na mbinu mpya ya kujinasua kwenye tatizo la kusuasua kwa miradi yake inayochangiwa na malimbikizo ya madeni kutoka kwa wateja yanayofikia zaidi ya Sh. bilioni 20.

Akizungumza jijini Arusha, mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Nehemia Mchechu, alisema mzigo wa madeni kutoka kwa wateja umechangiwa na majanga mbalimbali likiwamo wimbi la maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO-19, ambao umesababisha mdororo wa uchumi.

Alisema pamoja na tatizo hilo, NHC inaendelea kubuni mbinu mpya za kuzuia malimbikizo mapya ya kodi ya pango kuongezeka, lakini kuhakikisha kwamba malimbikizo ya nyuma yanaendelea kulipwa.

"Tumeshaanza kukutana na wadeni wetu ili kuweka utaratibu mzuri wa kumalizia madeni yao. Hivi sasa kuna mchakato unaendelea wa kuweka mifumo ya kielektroniki kwenye nyumba za shirika, ambao utawawezesha wateja wetu kulipia huduma wanazotumia bila kulimbikiza madeni,"alisema Mchechu.


Katika taarifa yake, Mkurugenzi huyo alifafanua kuwa hadi kufikia sasa NHC inadai malimbikizo ya zaidi ya Sh. bilioni 20 kutoka kwa wateja wake na kwamba malimbikizo hayo yameliathiri shirika kiasi cha kushindwa kufikia malengo yake iliyojipangia, ikiwamo kukamilisha miradi kwa wakati.

Kuhusu kuboresha rasilimali za NHC, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika hilo, Sophia Kongela, alisema nguvu kubwa kwa sasa imeelekezwa kufanya ukarabati wa nyumba za shirika hilo kote nchini na kuboresha miundombinu.

Aidha, Kongela alisisitiza kwamba tayari wameanza mchakato wa kuangalia uwezekano wa kuongeza ushirikishaji wa wadau wengine hasa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba, kipaumbele kikubwa kikielekezwa kwenye ujenzi wa nyumba za gharama nafuu.

Awali wakati anazindua bodi mpya ya shirika hilo jijini Arusha, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Anjelina Mabula, aliagiza watendaji wa shirika hilo kuongeza ubunifu na ushirikishaji katika kukabiliana matatizo yanayojitokeza.

Mabula alisema pamoja na kazi kubwa na nzuri inayofanywa na shirika hilo na matatizo yaliyoko, bado lina uwezo wa kufanya mambo makubwa zaidi kama kila mtendaji atatimiza wajibu wake.





Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ushetu, Gagi Lala, akifungua kikao cha Baraza la Madiwani ili kupitisha na kujadili rasimu ya mpango na bajeti ya matumizi wa mwaka fedha 2023/2024 hadi 2025/2026. Kushoto ni Makamu, Doa Limbu na Katibu wa Siasa na Uenezi Kahama, Joackimu Simbira, (kulia) ni Kaimu Mkurugenzi, Kakulima Deusi, kilichofanyika jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Madiwani wataka kasi ukusanyaji mapato

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamemtaka mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Linno Mwagenzi, kwa kushirikiana na watendaji kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na kufikia lengo la kukusanya Sh. bilioni 32.612.

Wakijadili mkutano maalumu wa Baraza la Madiwani kwa ajili ya kupitisha rasimu ya mpango na bajeti ya matumizi ya kawaida na mpango wa maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 hadi mwaka 2025/2026, Diwani wa Kinamapula, Sharifu Samweli alisema, fedha zinazotolewa na wahisani na ruzuku ya serikali ni nyingi kulinganisha na mapato ya ndani yanayokusanywa kila mwaka.

Alisema wakishindwa kufikia malengo miradi haitakamilika kwa wakati na vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu vitakosa mikopo.

Alisema wanatakiwa kukusanya Sh. bilioni 32.612 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kati ya hizo, Sh. bilioni 3.4 ni mapato ya ndani ya halmashauri yanayotokana na ushuru wa mazao na madini yaliyopo Kata ya Mwabomba na Sh. bilioni 29.16 ni ruzuku kutoka serikali pamoja na fedha za wahisani.

"Mwaka wa fedha 2021/2022 tulipanga kukusanya Sh. bilioni 31.1, lakini tulikusanya Sh. bilioni 29.7 pekee sawa na asilimia 96 ya makusanyo yote, bila kuongeza juhudi tutashindwa kufikia malengo na miradi yetu iliyoko kwenye kata itashindwa kukamilika na wananchi watakosa huduma ipasavyo," alisema Samwel.

Naye Diwani wa Viti Maalumu wa Kata ya Bulungwa, Ester Matone, alishauri kuziba mianya ya upotevu wa mapato hususani kupitia ushuru wa mazao pamoja na madini kwa kuwa baadhi ya watumishi wasiokuwa waadilifu wanachezea mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kusababisha halmashauri kukosa fedha.

Akitoa taarifa ya fedha, Ofisa Mipango wa halmashauri hiyo, Theresia Nsumba, alisema mwaka ujao wa fedha wanatarajia kukusanya na kutumia Sh. bilioni 32.6 kati ya hizo Sh. bilioni 3.4 ni mapato ya ndani na Sh. bilioni 29.1 ni ruzuku na fedha za wahisani ikilinganishwa na mwaka 2021/2022 walipanga kutumia Sh. bilioni 31.1 na kukusanya Sh. bilioni 29.7.

Alisema watahakikisha wanafikia malengo ya makusanyo kwa sababu kuanzia mwezi Desemba mpaka hivi sasa wameshakusanya Sh. bilioni 17.46 sawa na asilimia 46 na kuwataka madiwani kuhamasisha wananchi kwa kipindi hiki kulima mazao yanayohimili ukame ili halmashauri ipate mapato yake kupitia mazao.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alisema msimu huu wananchi wamelima mazao ya biashara na chakula kwa wingi na halmashauri itapata mapato yake ipasavyo na kufikia lengo.

Aliwataka wananchi kuacha kuuza chakula chote ili kukabiliana na njaa ndani ya familia.

# Kanisa lalaani mauaji katika jamii

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KANISA la Waadventista Wasabato, mkoani Shinyanga limelaani mauaji yanayoendelea eneo hilo na kuwaomba Watanzania wamrudie Mwenyezi Mungu ili waishi kwa upendo na amani.

Mchungaji wa Kanisa la Waadventista Wasabato Mtaa wa Sengerema, Brian Abdallah, alibainisha hayo juzi alipohitimisha siku 10 za maombi ya kurejea madhabahuni ambayo yalikuwa yakifanyika katika Kanisa la Wasabato mjini hapa.

Alisema katika maombi hayo yaliyoanza Januari 11 na kuhitimishwa juzi, wameliombea taifa amani pamoja na Watanzania wawe na hofu ya Mungu na kuacha kutenda maovu ikiwamo kuuana kikatili.

"Tumekuwa na siku 10 za maombi ya kurejea madhabahuni hapa Kanisa la Wasabato Shinyanga Mjini watu wa Mungu wamebarikiwa sana na katika maombi haya tunataka amani itawale kusiwapo tena na matukio ya mauaji wala ukatili wa kijinsia," alisema mchungaji Brian.

"Majuzi tu hapa kupitia vyombo vya habari tulisoma taarifa ya kusikitisha, mama mmoja ameuawa kikatili na kukutwa mtoto wake akinyonya maziwa yake huu ni unyama wa aina gani tunaomba watu wamrudie Mungu wao," aliongeza.

Naye Mchungaji wa Kanisa la Wasabato Shinyanga Mjini, Lazaro Mbogo, aliwataka Watanzania waishi kwa amani na upendo na kutoa mfano vita vya Ukraine na Urusi jinsi wananchi wa mataifa hayo wanavyoteseka.

Baadhi ya waumini wa kanisa hilo walisema maombi hayo ya siku 10 yamewajenga kiimani ili waendelee kuishi kwa amani na upendo.

## DC aonya wafanyabiashara walanguzi mahindi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAFANYABIASHARA wilayani hapa wametahadharishwa kununua mahindi ya ruzuku yanayotolewa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwa bei nafuu na kwenda kuwauzia wananchi vijijini kwa bei ya juu.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, wakati akizungumza na waandishi wa habari Kata ya Nyamilangano, Halmashauri ya Ushetu baada ya kuibuka malalamiko ya wananchi kuhusu kuwapo wafanyabiashara wanaonunua mahindi hayo na kwenda kuyauza kwa bei ya juu. Alisema serikali imetoa ruzuku ya mahindi na kuwauzia wananchi kwa bei ndogo ya kilo 20 kwa Sh. 15,000, lakini baadhi ya wafanyabiashara wanayanunua kwa bei hiyo na kwenda kuwauzia wananchi sokoni kwa Sh. 25,000.

Kiswaga alisema wafanyabiashara watakaobainika wakikununua mahindi hayo watafunguliwa mashtaka ya uhujumu uchumi kwa kitendo hicho kwa kuwa serikali inapambana kukabiliana na janga la njaa kwa kuwauzia wananchi wake mahindi kwa bei ndogo huku wengine wakinunua na kuyauza bei ya juu. "Msimu wa mwaka juzi wananchi walipata mahindi mengi shambani na kukosa soko hali iliyosababisha NFRA kuyanunua yote na kuyahifadhi na sasa inayarejesha kwa wananchi kwa kuwauzia kwa bei ndogo ya Sh. 15,000 kwa kilo 20 ukilinganisha na bei iliyoko sokoni ya Sh. 25,000," alisema Kiswaga.

Alisema kwa sasa wanafanya utaratibu wa kuyafikisha mahindi hayo katika kata zote 58 zilizoko wilayani Kahama ili kuwaondolea usumbufu wananchi wa kusafiri umbali mrefu kuyatafuta.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa katika ofisi za serikali za vijiji, mitaa na watendaji wa kata wanapouziwa bei kubwa na wafanyabiashara ili kuwachukulia hatua.

Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema msimu uliopita wananchi hawakupata mavuno mengi kutokana na mabadiliko ya tabianchi hali iliyosababisha kuomba msaada wa mahindi kukabiliana na njaa ndani ya familia.

Alisema awamu ya kwanza alipata tani 100 za mahindi ya ruzuku na yakauzwa kwa wananchi kwa bei ndogo ya Sh. 15,000 kwa kilo 20 tofauti na ile ya sokoni na kila mmoja alipata chakula cha kulisha familia yake na sasa amepata tena tani 400 ambazo zitawafikia wananchi katika kata zote 20 za halmashauri hiyo.

Naye mkazi wa kata ya Nyamilangano, Ester Godfrey, alisema baadhi ya wafanyabiashara wanawatuma watu kwenda kununua mahindi hayo na baadaye unayakuta sokoni yanauzwa kwa Sh. 25,000 kwa kilo 20.

# Nipashe Spotika



FIRMINO UK. 12-13



MBAPPE

# WACHEZAJI 5 WALIOFUNGA HAT-TRICK NYINGI 2022

**LONDON,** England

KUFUNGA mabao matatu 'hat-trick' na kuondoka na mpira nyumbani ni ndoto ya kila mshambuliaji kwenye uwanja wa mpira wa miguu. Kupata bao si rahisi katika soka, kwa hivyo kufunga mara tatu katika mchezo mmoja ni mafanikio makubwa.

Makala haya inawaangalia wachezaji watano kutoka ligi tano bora za Ulaya waliofunga hat-trick nyingi zaidi mwaka 2022, haya sasa...

**#5. Eldor Shomurodov - AS Roma**

Eldor Shomurodov ni jina la kushangaza kwenye orodha hii, kwani yeye si miongoni mwa wachezaji mashuhuri katika soka duniani. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uzbekistan alifunga hat-trick mbili mwaka jana.

Cristiano Ronaldo, Karim Benzema, Heung-Min Son, na Ivan Toney, ni miongoni mwa wengine, pia waliofunga hat-trick mbili mwaka 2022, lakini Shomurodov yuko juu yao kwa sababu alifunga katika mechi chache (35).

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ni nahodha wa Timu ya Taifa Uzbekistan na mmoja wapo wa safu ya ushambuliaji ya Jose Mourinho kule AS Roma.

Hat-trick zake hazikuja katika ngazi ya klabu, lakini kwenye hatua ya kimataifa. Alifunga bao lake la kwanza mwaka huu katika ushindi wa 4-2 wa kimataifa wa kirafiki dhidi ya Uganda. La pili lilikuja katika ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Maldives kwenye mechi ya kufuzu Kombe la Asia.

Mshambuliaji huyo wa Uzbekistan ameanza polepole msimu huu, akishiriki mara nane pekee na kufunga mara moja katika mashindano yote akiwa na Roma.

**#4. Victor Osimhen - Napoli**

Fowadi huyo wa Nigeria ni mmoja wa washambuliaji walio na viwango vya juu zaidi barani Ulaya kwa sasa. Victor Osimhen ndiye mfungaji bora wa Napoli msimu huu akiwa amefunga mabao 10 na asisti tatu katika mechi 15 za mashindano yote.

Mshambuliaji huyo mrefu, mtanashati na mwenye uwezo mkubwa, alifunga hat-trick na kufikisha mabao manne mwaka jana.

Alifunga mabao manne katika ushindi wa 10-0 wa Nigeria dhidi ya Sao Tome na Pricipe katika mechi ya kufuzu Kombe la Mataifa ya Afrika Juni mwaka jana. Pia alifunga mabao matatu katika ushindi wa 4-0 wa Napoli dhidi ya Sassuolo, Oktoba.

**#3. Robert Lewandowski - Bayern Munich / Barcelona**

Robert Lewandowski ni mmoja wa washambuliaji hodari katika soka. Fowadi huyo wa Poland ana ujuzi wa kufunga mabao na aliwahi kufunga mabao matano ndani ya dakika tisa pekee kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Mshindi huyo mara mbili wa Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya, aliwakilisha klabu mbili za mwaka 2022, Bayern Munich na Barcelona. Lewandowski alifunga hat-trick tatu.

Akiwa Bayern Munich, alifunga mabao matatu dhidi ya FC Cologne na RB Salzburg kwenye Bundesliga na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Pia alifunga mabao matatu katika mechi yake ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Barcelona dhidi ya Viktoria Plzen.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, kwa sasa ana mabao 18 na asisti nne katika mechi 20 kwenye mashindano yote ya msimu huu.

**#2. Erling Haaland - Borussia Dortmund / Manchester City**

Haishangazi kumuona Erling Haaland kwenye orodha kulingana na rekodi yake ya kufunga mabao. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alisajili mabao 46 katika michezo 43.

Mabao yake mwaka 2022 yalisajiliwa kwa Borussia Dortmund na Manchester City. Hat-trick yake ya kwanza mwaka huu ilikuwa kwenye Bundesliga dhidi ya VfL Bochum. Pia alifunga hat-trick mfululizo kwenye Ligi Kuu ya England dhidi ya Crystal Palace na Nottingham Forest na nyingine dhidi ya Manchester United.

Haaland amekuwa mzuri sana kwa Man City msimu huu akiwa na mabao 27 na asisti tatu katika michezo 22 hadi sasa.

**#1. Kylian Mbappe - Paris Saint-Germain (PSG)**

Mshambuliaji wa Ufaransa na PSG, Kylian Mbappe, ndiye mchezaji aliyefunga hat-trick nyingi zaidi mwaka 2022. Mbappe alifunga hat-trick tano kwa klabu na nchi yake katika mwaka uliomalizika.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ni mmoja wa wafungaji mahiri katika soka kwa sasa. Alifunga mabao 56 katika mechi 56, nyingi zaidi kuliko mchezaji yeyote mwaka 2022.

Mbappe alifunga hat-trick tatu kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1 na moja kwenye Coupe de France.

Mwisho wake wa mwaka ulikuja katika fainali ya Kombe la Dunia la FIFA la 2022 dhidi ya washindi Argentina, ambapo alifunga mara tatu.

## ISIKUPITE

TANGU kuanza kwa mwaka 2020 hadi sasa 2023, mshambuliaji wa Barcelona, Robert Lewandowski ndiye mchezaji wa soka mwenye mabao mengi zaidi (104) kwenye mechi za ligi akifuatiwa na Erling Haaland wa Manchester City (83) na Kylian Mbappe wa PSG (75).



## Extra Time

# MABEKI WA5 KIKWAZO KWA RONALDO NYAVUNI


RAMOS

**LONDON, England**

CRISTIANO Ronaldo anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora katika zama za kisasa. Rekodi ya Ronaldo inajieleza yenyewe jinsi nyota huyo wa Ureno alivyo mmoja wa wachezaji bora zaidi kuwahi kutokea duniani.

Ronaldo pia amebadilisha mchezo wake sana ili kukabiliana na umri. Alianza uchezaji wake kama winga mwenye kasi ambaye angeweza kufanya fujo dhidi ya safu ya ulinzi, lakini sasa anaangazia kuuweka mpira wavuni kwa ufanisi mkubwa.

Bado anaweza kuwapita wachezaji, lakini si kwa masafa aliyozoea. Mabeki bado wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii ili kubana harakati zake na kumzuia asifunge bao.

Kwa maelezo hayo, hawa hapa ni mabeki watano ambao wamefanikiwa kujilinda dhidi ya supastaa huyo wa zamani wa Manchester United kwa miaka mingi...

**#5. Sergio Ramos**

Moja ya faida za kuwa wachezaji wenzake na Ronaldo ni kwamba unajifunza jinsi anavyocheza. Sergio Ramos na Alvaro Arbeloa walitumia faida hiyo dhidi yake wakati Ureno ilipokutana na Hispania kwenye Euro 2012.

Ureno walikuwa wamebakisha hatua mbili pekee kufikia ndoto yao kulibeba kombe hilo walipokutana na Hispania katika hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo.

Hakukuwa na mikwaju yoyote iliyolenga lango kwani pande zote mbili zilichagua kucheza kwa kujilinda iwezekanavyo, lengo likiwa ni kutoruhusu kufungwa.

Ronaldo ni mchezaji mmoja anayeweza kuvunja msukosuko hata kama timu haichezi katika ubora wake. Lakini katika hafla hii, hakuweza kushawishi mchezo licha ya juhudi zake bora.

Hii kwa kiasi kikubwa ilitokana na jinsi Ramos na Arbeloa walivyoweza kumzuia. Hawakumpa nyota huyo wa Ureno mapumziko ya dakika moja na walimfanya anyamaze kwa muda wote.

**#4. Eric Abidal**

Eric Abidal alikuwa na kazi nzuri sana akiwa na Barcelona. Alikuwa sehemu ya kikosi maarufu cha Pep Guardiola ambacho kilishinda kila kitu katika njia yao. Moja ya usiku wake wa kukumbukwa ulikuja wakati yeye na timu ya Barcelona walipoirarua Real Madrid.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kukutana kati ya Jose Mourinho na Pep Guardiola kwenye La Liga. Real Madrid walisafiri hadi Camp Nou wakitaka kupunguza uongozi wa Wakatalunya hao.

Haikuwa mara ya kwanza kwa Ronaldo kukutana na Wakatalunya, lakini alinyamazishwa sana na walinzi. Barcelona walitawala sehemu kubwa ya umiliki wa mpira.

Mpinzani wa Ronaldo, Lionel Messi alikuwa na mchezo wa ajabu, wakati nyota huyo wa Ureno hakupewa nafasi au muda wa kufanya mashambulizi ya aina yoyote - shukrani kwa Abidal.

Mfaransa huyo alijua jinsi Ronaldo anavyoweza kuwa hatari kwenye winga. Hii ndiyo sababu alijitahidi sana kuhakikisha kwamba Ronaldo hapiti.

Usiku huo, safu ya nyuma ya nne iliwaweka kimya sana washambuliaji wa Real Madrid. Ulikuwa ni usiku ambao Ronaldo angetaka kuusahau. 'Los Blancos' walikumbana na kipigo cha mabao 5-0 kwenye mechi ya El Clasico, huku Abidal akijiweka sawa dhidi ya mmoja wa wachezaji bora katika soka duniani.

**#3. Alessandro Nesta**

Alessandro Nesta ni mmoja wa wachezaji waliopambwa zaidi na AC Milan kama beki mkubwa. Pamoja na Paolo Maldini, aliunda ushirikiano karibu usioweza kupenyeka nchini Italia.

Sir Alex Ferguson hakuwa na kawaida ya kupoteza mara nyingi sana, lakini dhidi ya Milan, timu yake ya Manchester United ilitolewa kabisa. Licha ya kujivunia Wachezaji kama Wayne Rooney, Cristiano Ronaldo na Ryan Giggs katika safu ya ushambuliaji, United hawakuwahi kuitisha timu ya AC Milan.

Nesta, siku hiyo, hakuwa na Maldini kando yake, lakini mabeki wengine walimpa sapoti ya kutosha kuisimamia safu ya ulinzi. Rooney na Ronaldo walizoea kubadilishana nafasi, lakini hakuna hata moja kati ya hizo iliyofanya kazi dhidi ya safu ya nyuma ya Milan.

Manchester United ilipeperushwa na timu ya Milan katika kipindi cha kwanza huku Clarence Seedorf akifunga mara mbili na kuwafanya wasonge mbele kwa mabao 2-0. United walimiliki mpira zaidi kipindi cha pili, lakini Ronaldo hakuweza hata kupiga shuti la maana lililolenga lango.

Milan walikuwa wameundwa kwa kiwango cha juu katika ulinzi na yote yalitokana na usomaji wa Nesta wa mchezo na ushirikiano na washirika wake wa ulinzi.

**#2. Ashley Cole**

Ashley Cole na Ronaldo walikutana mara kadhaa kwenye Ligi Kuu England.

Wakati Cole alipokuwa Arsenal, Ronaldo alikuwa kijana ambaye alicheza bila hofu. Ronaldo alikuwa bidhaa isiyojulikana wakati huo, ambayo ilifanya iwe vigumu kwa mabeki kumtabiri.

Hata hivyo, Cole alimrudisha wakati akiwa na Chelsea na hata wakati England ilipokutana na Ureno. Alijifunza jinsi ya kubadilisha hila za Ronaldo kwa kushikamana naye karibu iwezekanavyo na kimsingi kumtoa nje ya mchezo.

Ronaldo amewahi kusema kwamba, Cole ni mmoja kati ya wapinzani wagumu aliowahi kukutana nao.

"Kwa miaka mingi nilikuwa na vita kubwa na Ashley Cole, hakupi sekunde ya kupumua. Alikuwa mchezaji shupavu sana alipokuwa kwenye kilele chake, mwepesi, mgumu katika kukaba."

**#1. Diego Godin**

Atletico Madrid, chini ya Diego Simeone, imekuwa na nguvu ya kutegemewa, ndani na pia Ulaya. 'Rojiblancos' hao wanajivunia rekodi nzuri sana dhidi ya wapinzani wao wa jiji chini ya El Cholo.

Mchezaji mmoja, haswa, amepata sifa kubwa kutoka kwa wachambuzi kote ulimwenguni kwa ubora wake katika safu ya ulinzi. Diego Godin, enzi zake katika mji mkuu wa Hispania, alikuwa mwamba wa Atletico Madrid, kwani aliisaidia timu hiyo kupata sifa ya kuwa moja ya timu ngumu zaidi kuifunga Ulaya

Real Madrid waligundua mara kadhaa dhidi ya majirani zao jinsi ilivyo ngumu kuwashinda. Kando na fainali za Ligi ya Mabingwa Ulaya 'Los Blancos', katika misimu ya hivi karibuni, hawajapenda kucheza Atletico.

Moja ya mechi mbaya zaidi ya Ronaldo ilikuja dhidi ya Atletico mnamo mwaka 2015 walipochapwa mabao 4-0 ugenini. Ronaldo alipata mshtuko, baada ya kutolewa nje ya mchezo na walinzi wa Atletico.

Los Blancos walikuwa na mashuti manne pekee yaliyolenga lango, huku moja pekee likilenga lango. Ronaldo alilipiza kisasi msimu uliofuata kwa kufunga hat-trick dhidi ya Atletico.

## Nukuu

"Inapendeza kucheza soka la kiwango cha juu hapa na wachezaji wazuri. Nina furaha hapa na ninakusudia kubaki hapa na kusaidia Liverpool," **Roberto Firmino wakati huu mkataba wake hapo Anfield ukitarajiwa kumalizika Juni mwaka huu.**



"Tunazungumza kuhusu mmoja wa makocha bora katika historia, Sir Alex na kijana kutoka Arsenal. Ni zama tofauti, soka tofauti. Soka limebadilika kidogo, lakini ngoja tuone. Makocha wote wawili ni wazuri sana kwa sasa, wanacheza vizuri na utakuwa mchezo mzuri," **Kipa wa Manchester United, David De Gea, akikataa kufananisha vita vya kocha wao sasa, Erik ten Hag na Mikel Arteta wa Arsenal kama ilivyokuwa enzi za Ferguson na Arsene Wenger, kabla mchezo wao wa jana usiku.**



"Nilishinda La Liga mara nne mfululizo nikiwa mchezaji. Msimu wa tano sikuwa sawa, wa sita sikuwa sawa. Sikuwa na njaa ya kutosha. Niliwaza 'Niko vizuri sana' na Madrid wakanishinda mara ya tano na sita. Ninaelewa (changamoto) lakini niko hapa kuifanya. Mwenyekiti anajua hilo, nataka kuwa hapa, vinginevyo sitasaini, lakini nikipoteza timu au nikipoteza kitu siwezi kuwa hapa. Hapa watu hawasubiri. Tunashika nafasi ya pili kwenye msimamo hatuko nyuma ya Arsenal kwa pointi 25," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, akifunguka kuhusu kuachia ngazi.**






# MASTAA WALIOISHIA KUTAJWA USAJILI WA DIRISHA DOGO BARA

Na Adam Fungamwango

PRESHA za mashabiki wa soka nchini sasa zimeshuka baada ya dirisha dogo la usajili kufungwa. Kila siku walikuwa wakikodolea macho kwenye mitandao ya kijamii, televisheni na magazeti kuangalia ni mchezaji wao amesajiliwa na klabu gani.

Presha zaidi ilikuwa kwa mashabiki wa klabu kubwa kongwe za Simba na Yanga ambazo waliamini kuwa vikosi vyao vinahitaji wachezaji wa kuongeza nguvu katika michuano ya kimataifa.

Akili zao sasa watazielekeza kwenye Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Kwa uchache tu nikizitaja klabu tatu za Ligi Kuu, mpaka zinafungwa, Simba ilikuwa imesajili wachezaji wanne ambao ni straika Jean Baleke mchezaji wa TP Mazembe aliyekuwa akichezea kwa mkopo Klabu ya Nejmeh ya Lebanon kiungo mkabaji Ismael Sawadogo kutoka Difaa El Jadida ya Morocco, straika kinda kutoka KMKM, Mohamed Mussa na mchezaji wa kwanza kabisa kusajiliwa na klabu hiyo, kiungo mshambuliaji raia wa Burundi, Saido Ntibazonkiza.

Yanga nayo ikafanya ingizo la wachezaji wanne ambao ni straika Kennedy Musonda kutoka Power Dynamos ya Zambia, beki wa kati Mamadou Doumbia kutoka Stade Malien ya Mali, golikipa Metacha Mnata kutoka Singida Big Stars na Mudathir Yahaya ambaye alikuwa mchezaji huru, huku Azam ikimshusha kipa Abdulai Iddrisu kutoka nchini Ghana.

Hata hivyo kulikuwa na tetesi nyingi na za wachezaji wengi ambao mpaka dirisha linafungwa hawakusajiliwa na timu hizo kama ambavyo mashabiki wengi walivyokuwa wakidhani kutokana na kutajwa sana kwenye nyanzo mbalimbali vya habari.

**Cesar Manzoki**

Tangu dirisha kubwa la usajili, huyu ndiye mchezaji anayetajwa na kuimbwa zaidi kwenye usajili wa vipindi vyote viwili. Alitajwa kuwa angejiunga na Simba mwanzoni mwa msimu huu, lakini haikuwa hivyo. Akajiunga na Dalian FC ya China na ikasemekana amepelekwa huko ili iwe rahisi kutwaa taji kuliko kwenye klabu yake ya zamani ya Vipers FC ya Uganda ambao walikomaa na kutaka kiasi kikubwa cha pesa kuliko uhalisia kwani mkataba wa mchezaji ulikuwa unaelekea ukingoni, hivyo ndoto za mashabiki kumuona Simba, zikatoweka.

**Feisal Salum 'Fei Toto'**

Mpaka sasa bado ni mchezaji wa Yanga, lakini kipindi kilichomalizika cha dirisha dogo alikuwa akihusishwa kwenda Azam FC, ingawa mara kwa mara viongozi wa klabu hiyo walikuwa wakikanusha.

Feisal Salum, kiungo mshambuliaji anayeichezea Zanzibar Heroes na Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, aliandika barua ya kuaga, huku akiununua mkataba wake. Akaingiza kiasi cha pesa kwenye akaunti ya klabu yake ambacho aliamini ni kipengele cha kufunja mkataba. Yanga ilizirudisha pesa hizo na kusema mchezaji huyo bado ni mali yao.

Sakata likahamia kwenye Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ambao walisema ni mchezaji halali wa Yanga.

Bado mchezaji huyo hajaripoti kambini, yeye na wanasheria wake wakiamini kuwa hawakutendewa haki, taarifa zikidai huenda wakalipeleka Mahakama ya Usuluhishi wa mambo ya Michezo duniani (CAS)

**Bobosi Byaruhanga**

Awali, alihusishwa kujiunga na Simba, lakini tetesi zikageuka na kudaiwa angejiunga na Klabu ya Yanga, hasa baada ya sakata la Fei Toto kuwa moto. Ikadaiwa kuwa ndiye angekuja kuwa mrithi wake kama mambo hayataenda vizuri. Huyu alikuwa kiungo mshambuliaji wa Vipers ya Uganda ambaye alizitoa udenda klabu za hapa nchini.

Wakati uvumi wa mchezaji huyo kujiunga na Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga ukishika kasi, ghafla zikatoka taarifa kuwa amejiunga na Klabu ya MFK Vyskov ya Czech ambayo nayo imempeleka Klabu ya Austin FC ya Marekani kwa mkopo utakaomalizika Novemba 30, mwaka huu.

**Luis Miquissone**

Bado hajaondoka kwenye mawazo na midomo ya mashabiki wa soka nchini. Kiungo huyu mshambuliaji wa zamani wa Simba ambaye baadaye akasajiliwa na Al Ahly ya Misri na kwa sasa anapelekwa kwenye klabu mbalimbali kwa mkopo, alitajwa sana kujiunga na Yanga.

Japo mwanzoni kwa kipindi cha dirisha dogo ilisemakana kuwa angerejea kwenye klabu yake ya zamani, lakini Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Salim Abdallah 'Try Again' akawaambia wanachama na mashabiki wa Simba kuwa hawana mpango huo na Luis Miquissone ni mchezaji halali wa Al Ahly. Baada ya hapo stori zikahamia kwa watani zao wa jadi, Yanga. Cha ajabu hata baadhi ya maofisa wa klabu hiyo wakawa wanaweka picha ya mchezaji huyo kwenye kurasa zao za mitandao ya kijamii, wakionyesha kwamba kuna kitu kitafanyika kuhusu raia huyo wa Msumbiji. Dirisha limefungwa na stori zikaishia hapo. Zilikuwa mbwembwe tu na kurushana roho.

**Jean-Marc Makusu**

Straika huyu raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo naye safari hii alikuwa kwenye orodha ya wachezaji waliotajwa kusajiliwa na timu za Ligi Kuu Tanzania Bara. Klabu ya Simba ndiyo iliyohusishwa na mchezaji huyo Jean Makusu ambaye anaichezea DC Motema Pembe na alicheza mechi za Kombe la Shirikisho barani Afrika na mabao yake yalichangia kuipeleka timu hiyo hatua ya makundi.

Wadadisi wa masuala ya soka wakawa wanajiuliza, iwapo Simba itamsajili mchezaji huyo itakuwaje? Kwa sababu za kikanuni hatoweza kuichezea timu hiyo Ligi ya Mabingwa, zaidi ya Ligi Kuu na Kombe la FA tu. Je, Simba haitoongeza straika kwa ajili ya Ligi ya Mabingwa zaidi ya kwenye ligi tu? Wakasubiri waone. Simba ikamshusha raia wa huko huko Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Jean Baleke. Huyu ana sifa ya kucheza Ligi ya Mabingwa kwa sababu alikuwa akicheza soka nchini Lebanon kwa mkopo Klabu ya Nejmeh akitokea TP Mazembe. Hajacheza ligi yoyote inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) msimu huu. Habari za Makusu zikafungwa rasmi.

**JE, WAJUA?**



Manchester City ndiyo klabu iliyoingiza mapato makubwa zaidi (Euro milioni 731) kwa mwaka 2022, ikifuatiwa na Real Madrid (Euro milioni 713.8) na Liverpool (Euro milioni 701.7).





# Watumishi wanaosababisha upotevu wa mapato waonywa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, amesema hatawavumilia watumishi wa halmashauri hiyo watakaosababisha upotevu wa mapato.

Aliyasema hayo jana alipokuwa akitoa mapendekezo ya rasimu ya mpango wa bajeti kwa mwaka 2023/24 kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Jiji hilo.

Alisema baraza hilo limepitisha rasimu ya makisio ya mpango na bajeti kwa Jiji la Dodoma kwa mwaka 2023/24 na Sh.milioni 128.2 ni kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo na utoaji wa huduma, hivyo hataraji watumishi kusababisha upotevu wa mapato.

"Kutokana na fedha hizi zilizopitishwa ninawataka watumishi ambao watasababisha upotevu wa mapato sitawavumilia nitachukua hatua ili kuleta nidhamu wa ukusanyaji na matumizi," alisema.

Kadhalika, alisema kwa mwaka 2023/24 halmashauri hiyo imejiwekea msisitizo mkubwa katika kuhakikisha inakusanya mapato yake kama ilivyokasimia ili ilingane na utekelezaji wake.

Alisema mikakati mingine ya halmashauri hiyo ni pamoja na kutenga asilimia 60 kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikijumuisha asilimia 10 kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Alisema asilimia 10 ni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA).

Naye Meya wa Jiji hilo, Prof. Davis Mwamfupe, aliwataka madiwani hao kuhakikisha bajeti iliyopitishwa inatumika kama ilivyokusudiwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na si vinginevyo.

# Nape: Serikali imefanya makubwa kwenye sekta ya mawasiliano

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya mawasilino, hivyo na kujipa jukumu la kuwa kitovu cha biashara mtandao barani Afrika.

Aliyasema hayo juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Posta Afrika yaliyofanyika kwa siku mbili jijini hapo.

"Serikali imechukua hatua kubwa kuwekeza kwenye sekta ya mawasiliano nchini ikiwamo utekelezaji wa zoezi la anwani za makazi pamoja na kuwekeza fedha nyingi katika mkongo wa taifa," alisema Nnauye.

Aidha, alisema jitihada zingine zilizofanywa na serikali ni pamoja na kuandaa sheria, kanuni na taratibu za kuendesha biashara mtandao pamoja na kutungwa kwa Sera ya TEHAMA ya mwaka 2016.

Alisema kutokana na hali hiyo wizara yake inaendelea kuweka mikakati madhubuti ambayo italiwezesha kuwa kitovu cha biashara mtandaoni katika Bara la Afrika. "Hivi sasa kuna laini za simu milioni 58 na kati ya hizo milioni 40 zinatumika katika huduma za fedha, nichuke fursa hii kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa nia yake ya kuwezesha sekta hii ya mawasiliano nchini,"alisema.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa ofisi ya Makamu Mkuu ya Shirika la Posta Afrika jijini Arusha, Nape alisema serikali itahakikisha inatoa ushirikiano ili ukamilike kwa wakati.

"Tunawashukuru sana Shirika la Posta Afrika kwa kuichagua Tanzania kujenga jengo la makao makuu yake na kwa niaba ya serikali tunawaahidi kuwa tutatoa ushirikiano wetu wote ili ujenzi huu usiwe na changamoto yoyote na ukamilike kwa wakati,"alisema Nnauye.

Mkurugenzi wa Masuala ya Mawasiliano kutoka Mamalaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Emmanuel Mannasseh, alisema wataendelea kuweka mazingira na sera muafaka ili kuwawezesha vijana kushiriki na kunufaika na ukuaji wa uchumi wa kidijitali.

"Kwa kuwa serikali inafanya kazi muda wote kutafuta na kuwekeza fedha nyingi ili kusaidia kuboresha upatikanaji wa miundombinu inayohitajika kwa ajili ya upanuzi wa uchumi wa kidijitali ni jambo la busara kwa vijana kutambua na kujitosa katika sekta hiyo," alisema.

Aliongeza kuwa uboreshaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ulikuwa na mchango mkubwa katika kuharakisha utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi nchini.

Pia alisisitiza kuwa iwapo itatumiwa kwa busara, sekta hiyo itasaidia Watanzania wengi kujikwamua na minyororo ya umaskini ikiwamo kupunguza ongezeko la kiwango cha ukosefu wa ajira.

"Ningependa kutoa changamoto kwa vijana kote nchini kufikiria juu ya njia za kuvuna kutokana na fursa nyingi za kiuchumi ambazo uchumi wa kidijitali unakaribia, hasa kwa kuunda huduma yoyote muhimu ya kidijitali inayotoa majukwaa," alisisitiza.




Meneja Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Shirika la Amref, Mhandisi Mturi James (wa pili kulia), akimkabidhi Mganga Mkuu wa Jiji la Dodoma, Dk. Andrew Method, vifaa vya kunawa mikono kwa ajili ya kujikinga na magonjwa ambukizi kwa kata 41 za halmashauri hiyo. Shirika hilo lilikabidhi vifaa 5,000 vya thamani ya Sh. milioni 100 jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Watendaji waagizwa kutatua kero, kuchochea maendeleo

**Na Piter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), George Simbachawene, amewaagiza watendaji wa serikali kuendelea kutatua kero za wananchi zinazowakabili ili kuchochea kasi ya maendeleo hapa nchini.

Aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya siku mbili ya kujenga uwezo kwa Menejimenti ya Ofisi ya Waziri Mkuu yaliyolenga kuwajengea uelewa kuhusu idara ya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa shughuli za serikalini jijini hapo.

Aliwataka watendaji wa serikali kuhakikisha wanatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kutatua kero zinazowakabili wananchi katika maeneo yao.

Alisema kuwa ni muhimu kwa watendaji kuwajibika kwa kuyafikia malengo ya serikali na kuleta matokeo chanya.

"Hakikisheni mnakuwa watu wa msaada kwa wengine katika kuyatekeleza majukumu yenu, muwe watengeneza furaha na hii iwe kipimo kwa kila mwenye kukufikia huku ukizingatia taratibu za utumishi wa umma na sheria zilizoko," alisema.

Kadhalika, aliwaasa waendelee kutumia taaluma zao kuleta matokeo chanya kwa serikali na jamii na wakijitathmini utendaji wa kila siku wa kuwatumikia Watanzania.

"Ni sahihi kujitathmini kila iitwapo leo ili kuona namna unavyoleta matokeo chanya kwenye utendaji wako wa kila siku, matokeo utayoyapata yatatusaidia kuongeza tija," alisisitiza Waziri Simbachawene.

Alisema kuwa matokeo ya mafunzo hayo yatumike kuboresha mifumo ya uratibu, usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za serikali ili kuwa na uwezo wa kupima utendaji wa wizara na taasisi mbalimbali za serikali kisayansi.

Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Dk. John Jingu, alisema mafunzo hayo yanalenga watendaji wa serikali kufanya kazi kwa ufanisi.





# Jeshi la Polisi lafanya usafi mitaani kudhibiti magonjwa ya mlipuko

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limejitosa kufanya usafi katika maeneo mbalimbali mkoani hapa kwa lengo la kuyafanya mazingira kuwa safi na kuwaepusha wananchi na magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu.

Juzi askari zaidi ya 200 wa jeshi hilo walisambaa katika maeneo mbalimbali ya Jiji hilo yakiwamo maeneo yenye mikusanyiko ya watu kufanya usafi ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Polisi na Jamii.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi Benjamin Kuzaga alisema utaratibu huo wa kufanya usafi ilikuwa ni miongoni mwa maagizo ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Camillus Wambura.

Alisema mbali na kuyafanya maeneo ya Jiji hilo kuwa safi lakini pia walikuwa wanalenga kuimarisha ushirikiano na jamii katika kushughulikia mambo mbalimbali ya kijamii.

Alisema walilenga kusafisha mitaro ya maji, kufyeka nyasi na vichaka visivyotakiwa, kusafisha maeneo ya umma ikiwamo vituo vya mabasi, sokoni na kwenye vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya.

"Lengo letu ni kuionyesha jamii mfano ili nayo ishiriki kikamilifu kwenye usafi huu, kwa leo tunafanya usafi huu kutokana na maagizo ya Mkuu wa Jeshi la Polisi lakini tuko tayari kushirikiana na jami kufanya usafi huu kila mwezi mara moja," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema jeshi hilo ni miongoni mwa taasisi zinazozalisha taka na hivyo ni wajibu wao kushiriki kuziondoa ili kuepuka madhara yanayotokana na uchafu huo akieleza kuwa madhara yanaweza yakawakumba pia maaskari.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua ambaye ndiye alizindua usafi huo aliwapongeza maaskari hao kwa kujitokeza kwa wingi kufanya usafi huo huku akizitaka taasisi zingine za umma kuiga mfano huo wa kujitolea.

Pia alimshukuru Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini kwa kutoa maelekezo ambayo yaliwafanya maaskari kujitokeza na kufanya kazi hiyo ya kijamii ndani ya wilaya yake.

Dk. Chuachua aliwataka wananchi kushirikiana na kamati zilizoundwa kwenye maeneo yao kwa ajili ya kusimamia usafi ili kuhakikisha Jiji hilo linakuwa na hadhi inayostahili badala ya kuwa chafu kama ilivyokuwa miezi kadhaa iliyopita.

"Lakini niwatake pia madiwani wa Jiji la Mbeya waendelee kusimamia usafi kwenye maeneo yao, usafi ni miongoni mwa vipaumbele vya Jiji letu, sasa tumeshapeana maelekezo na kinachotakiwa sasa hivi ni utekelezaji tu," alisema Dk. Chuachua.

Alisema Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo iliagiza Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji hilo kuajiri kampuni ambazo zitakuwa zinafanya usafi kwenye maeneo ya kata mbalimbali baada ya utaratibu wa zamani wa kutumia maghuba kusitishwa.

Mkuu wa Kitengo cha Udhibiti Taka wa Jiji la Mbeya, Nimroad Kapoloza, alisema halmashauri hiyo iliondokana na matumizi ya maghuba ya kubebwa na magari baada ya kubaini kuwa utaratibu huo ulikuwa hauna tija. Alisema utaratibu huo ulikuwa unachangia mrundikano wa taka kwenye maeneo mbalimbali kutokana kutokuwa na uwezo wa kuyaondoa kwa wakati yanapokuwa yanajaa.

Alisema tatizo hilo lilikuwa linasababishwa na uhaba wa magari ya kubebea maghuba hayo akieleza kuwa kwa halmashauri ilikuwa na magari matatu ambayo yalikuwa na uwezo wa kuondosha maghuba 20 mpaka 30 kwa wiki wakati uzalishaji wa taka ilikuwa ni maghuba 40 kwa wiki.

Alisema baada ya kuanzisha utaratibu mpya wa kila kata kujitegemea, hali ya usafi imeanza kutengamaa kwa maelezo kuwa kwenye baadhi ya kata wameajiri kampuni ya kuzoa taka na kwenye maeneo mengine kata zinajitegemea.

Alisema baada ya kuanzisha utaratibu huo mpya, magari ya kuzoa taka yameongezeka kutoka matatu yaliyokuwa yanatumika mpaka 28 ambayo kila kata inayofanya usafi ina gari moja.

# DC atangaza msako kwa wanafunzi wasioripoti shuleni

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, imetangaza kuanzisha operesheni maalumu ya kuwasaka wanafunzi waliofaulu darasa la saba na kutakiwa kujiunga kidato cha kwanza lakini hawajaripoti shuleni mpaka sasa.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, alitangaza kuanza kwa operesheni hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu wilayani humo. Alisema wapo wanafunzi wengi wa kidato cha kwanza ambao mpaka sasa hawajaanza masomo bila taarifa yoyote na hawajulikani waliko jambo ambalo alisema linakwamisha maendeleo ya elimu.

Alisema kwa sasa serikali inaendelea na utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo, hivyo hakuna sababu ya mzazi yeyote kutompeleka mtoto wake shuleni.

Alisema kitendo cha kutowapeleka watoto hao shuleni kinachochea ajira za utotoni hasa kwenye kilimo, ufugaji na shughuli za uchimbaji madini ambazo ndizo shughuli kuu za kiuchumi kwa wilaya hiyo.

Aliwataka walimu kuendelea kuwapokea watoto wote hata kama bado hawana sare za shule ili waendelee kusoma wakati vifaa hivyo vinatafutwa.



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya ambaye ni Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi (katikati), akikabidhi vifaa vya TEHAMA kwa uongozi wa Shule ya Msingi Iwambi ya jijini Mbeya kwa ajili ya kurahisisha shughuli mbalimbali za shule hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Shule ya Msingi Iwambi yapewa msaada wa vifaa vya TEHAMA

**Na Nebart Msokwa**, MBEYA

NAIBU Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, amekabidhi vifaa vya TEHAMA katika Shule ya Msingi Iwambi ya jijini Mbeya kwa ajili ya kurahisisha shughuli mbalimbali zinazohitaji teknolojia ikiwamo uchapishaji wa mitihani na majaribio mbalimbali.

Vifaa vilivyokabidhiwa na mbunge huyo ni kompyuta pamoja na mashine ya kudurufu maandishi ambavyo ndivyo vilivyokuwa vinahitajika shuleni hapo.

Mahundi alikabidhi vifaa hivyo mwishoni mwa wiki ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyotoa mwaka jana aliposhiriki kupanda miti shuleni hapo kwa kushirikiana na kikundi cha Iwambi Active Group kinachofanya shughuli mbalimbali za kijamii.

Mahundi ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya alisema pamoja na kwamba aliahidi kutoa vifaa hivyo pia ni sehemu ya kumuunga mkono Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye amedhamiria kuboresha elimu nchini.

Alisema serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwenye sekta ya elimu zikiwamo za kuboreshea miundombinu na za uendeshaji wa eimu bila malipo inayoendelea kwa sasa kuanzia darasa la awali mpaka kidato cha sita.

"Nitahakikisha nasaidia sekta ya elimu ili wazaliwe wahandisi wengi kama mimi, wazaliwe madaktari, wazaliwe wataalamu wa kilimo na wataalamu wengine kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu," alisema Mahundi.

Hata hivyo Mahundi aliwataka wananchi kumuunga mkono Rais Dk. Samia katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo amekuwa akisisitiza kila siku ikiwamo ya elimu, maji, barabara, afya na sekta zingine muhimu.

Akipokea vifaa hivyo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Iwambi, Eliah Kasanga, alisema vifaa hivyo vitasaidia kutunza nyaraka za shule sambamba na kudurufu mitihani ambayo walikuwa wakichapa mitaani.

Alisema kitendo cha kuchapa na kudurufu mitihani na nyaraka zingine za shule ni gharama kubwa kuliko watakapokuwa wanafanyia shughuli hizo shuleni.

"Baadhi ya nyaraka tunazochapisha ni za siri, kwa hiyo kitendo cha kuchapisha mtaani kinaweza kusababisha baadhi ya siri kuvuja jambo ambalo sio zuri, kwahiyo tunakushukuru sana Naibu Waziri kwa kutusaidia vifaa hivi," alisema Mwalimu Kasanga.

Mratibu Elimu Kata ya Iwambi, Mwalimu Gilbert Kasebele, alisema shule nyingi katika kata yake zinakabiliwa na matatizo mbalimbali, hivyo akawaomba wadau mbalimbali wa elimu mkoani humo kuendelea kusaidia.

Alisema shule nyingi hazina vifaa vya TEHAMA ambavyo kwa dunia ya sasa ni muhimu, hivyo akaeleza kwamba msaada uliotolewa umesaidia kupunguza tatizo.

Diwani wa Kata ya Iwambi, Humphery Ngalawa, alimshukuru Mahundi kwa moyo wake wa kujitolea na akamtaka asichoke kuendelea kusaidia maeneo mengine yenye uhitaji.



# Mwinyi awataka wahitimu kufanya utafiti ufumbuzi matatizo ya jamii

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wahitimu wa vyuo vikuu kujikita na utafiti utakaotoa ufumbuzi wa matatizo kwenye jamii.

Alivitaka vyuo vikuu kuongeza fani kwa mujibu wa mahitaji ya wakati uliopo na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani ili kuleta mabadiliko nchini.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo kwenye sherehe za Mahafali ya 22 ya Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al- Sumait, Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar.

Aliwataka wahitimu hao kutumia utafiti kwa lengo la kutatua changamoto kwenye jamii badala ya kuziweka kwenye maktaba na kuzifungia.

Alizishauri wizara na idara za serikali kushirikiana na vyuo vikuu kufanya utafiti wa kuchochea maendeleo kwenye nyanja zote za jamii na uchumi, TEHAMA na mawasiliano ili kuleta mabadiliko yenye tija.

"Nazishauri wizara na idara za serikali kushirikiana na wataalamu wa vyuo vikuu, kufanya tafiti zitakazosaidia kuchochea maendeleo katika nyanja za kijamii, uchumi na teknolojia ya habari na mawasiliano ili kuendelea kusonga mbele," alisema.

Hata hivyo, aliwasihi wahitimu watakao bahatika kuajiriwa ama kujiajiri baada ya kuhitimu mafunzo yao, wakafanye kazi kwa uadilifu, kujituma na kuchunga maadili katika jamii zao, kwa kuleta mabadiliko kwenye utendaji wao. Aliwataka wakawe wabunifu wa kuzitafuta fursa na kuzitumia ili wajiendeleze kwa weledi na ufanisi wa hali ya juu kwa lengo la kujiimarisha kitaaluma.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina nia ya kutanua wigo kwenye shule za umma kwa kuweka kipaumbele kwenye mafunzo ya amali ya ufundi ili kuwapa uwezo wanafunzi wanaomaliza masomo yao wajiajiri.

Alisema Sera ya Elimu inawataka wanafunzi watakapomaliza masomo yao ya lazima kwa ngazi ya sekondari, kuwe na sehemu ya kujiendeleza kwa stadi za ufundi na vitendo.

"Lazima tuwe na taasisi, tuwe na vyuo vyenye kutoa fani tofauti ambazo wanafunzi watajiajiri baada ya masomo yao," alishauri Waziri Lela.

Naye Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Msafiri Mshewa, aliwataka wahitimu hao wakasaidie kuleta mabadiliko chanya kwenye jamii zao kwa kutumia vizuri ujuzi wa taaluma zao kuongeza tija na wawe mabalozi wazuri wa kuzikimbilia fursa kwa kuzifanyia kazi zenye tija.

"Ni matumaini yetu elimu mliyoipata itawanufaisha nyinyi, jamii na Watanzania kwa ujumla, kila mmoja wenu ana wajibu na nafasi ya kuchangia maendeleo kwa kuangalia eneo la taaluma yake litakavyosaidia kuleta mageuzi ya maendeleo kwa kuajiriwa ama kujiajiri wenyewe."

Jumla ya wahitimu 310 wakiwamo wanawake 183 na wanaume 127 walihitimu masomo yao.

Wahitimu 18 kati yao walitunukiwa shahada ya udhamili, 241 shahada ya kwanza na 51 walitunukiwa stashahada na astashahada.



Baadhi ya Masheha wa Wilaya ya Kusini Unguja wakimsikiliza Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Rahma Kassim Ali (hayupo pichani), katika kikao cha pamoja cha kujadili migogoro ya ardhi kilichofanyika ofisi ya wilaya hiyo Makunduchi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Uvamizi, uuzaji holela chanzo migogoro ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar imesema kumekuwa na uvamizi na uuzaji holela wa maeneo ya ardhi ya akiba na kuchangia ongezeko la migogoro kisiwani hapo.

Hayo yalisemwa jana na waziri wa wizara hiyo Rahma Kassim Ali, alipokutana na Masheha wa Wilaya ya Kusini Unguja, katika kikao maalum kilichofanyika ofisi za mkuu wa wilaya hiyo, Makunduchi. Alisema wizara yake itahakikisha inaweka mikakati imara ya udhibiti wa uuzaji ardhi holela hasa katika maeneo ya akiba yaliyotengwa na serikali.

Alisema Wilaya ya Kusini Unguja inaongoza kwa uvamizi na uuzaji wa ardhi kiholela hasa katika maeneo ya fukwe za bahari yiliyo wazi na kutokana wizara yake kupewa dhamana ya usimamizi wa ardhi kwa mujibu wa tangazo la kisheria namba 137 ya mwaka 2020 itahakikisha inayadhibiti maeneo hayo.

"Wilaya ya Kusini Unguja, inaongoza kwa uvamizi na uuzaji wa maeneo kiholela hasa maeneo ya fukwe na yaliyo wazi, hivyo kwa vile wizara yangu ndiyo iliyopewa dhamana ya usimamizi wa ardhi kwa mujibu wa sheria nitahakikisha ninayadhibiti maeneo hayo na atakayebainikia kwenda kinyume hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake," alisema.

Aliwataka masheha hao kuunga mkono juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika usimamizi wa masuala ya ardhi pamoja na kufanya kazi zao ipasavyo kwa kutojihusiha na vitendo vya uuzaji wa ardhi bila kufuata sheria.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo Mzee Ali Haji alitoa ufafanuzi kuhusu matumizi ya ardhi kwa wageni na kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi namba 12 ya mwaka 1992 imekataza kuuziwa ardhi mgeni yeyote bali atatakiwa kukodishwa kwa ajili ya uwekezaji.

Mkurugenzi Mipango Miji na Vijiji Kutoka Kamisheni ya Ardhi, Muchi Juma Ameir, alisema Kamisheni ya Ardhi imeyaainisha maeneo yote yenye ardhi ya akiba katika Mkoa wa Kusini Unguja yakiwamo Paje, Muungoni na Muyuni kwa lengo la kuyapanga na kuyapima kwa kuyawekea alama na kuyadhibiti ili yasivamiwe kwa uuzaji wa viwanja.

Sheha wa Shehia ya Paje, Mohammed Rajabu Makame, alisema wanasheria ndiyo wanaohusika na masuala ya ukiukwaji wa sheria kwa kufanya vitendo hivyo na hata wao kuwakosesha ufanisi mzuri wa kiutendaji hasa katika kazi zao za usheha.

Mkuu wa Wilaya ya Kusini, Rajab Mkasaba aliwataka masheha kuwa mabalozi wazuri wa kutoa elimu kwa jamii kuhusu umiliki wa ardhi katika shehia zao.

Kikao hicho kimefanyika kwa lengo la kujadili na kuweka mipango mikakati ya usimamizi madhubutu ambao utasaidia kuondoa changamoto ya uuzaji wa ardhi kiholela pamoja na kupunguza migogoro ya ardhi nchini.

## Maeneo 46 kwenye tishio la mabadiliko tabianchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZAIDI ya maeneo 46 katika kisiwa cha Pemba yamebainika kuwamo kwenye tishio la athari ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuingiliwa na maji ya chumvi na wananchi kushindwa kuendelea na shughuli za kilimo.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Daima Mkali Moto, alisema hayo juzi wakati alipokuwa akitoa taarifa mbele ya kamati ya Baraza la Wawakilishi ya viongozi wakuu wa kitaifa kuhusu hali ya mabadiliko ya tabianchi yalivyoathiri eneo la Ndagoni, Wilaya ya Chakechake, Pemba.

Alisema juhudi mbalimbali zimechukuliwa na serikali na wananchi ikiwamo kujenga matuta ya kuzuia maji ya bahari kuingia katika maeneo ya kilimo na makazi.

Alisema shughuli za kilimo ikiwamo cha mpunga zimesita katika baadhi ya maeneo ya Ndagoni hadi Chakechake kutokana na kasi ya maji ya bahari kuingia katika maeneo ya mashamba ya kilimo.

Alizitaja baadhi ya athari hizo zimesababishwa kwa kiwango kikubwa cha shughuli za kijamii za binadamu ikiwamo ukataji wa miti aina ya mikoko ambayo kwa kiasi kikubwa husaidia kupunguza maji ya bahari kujaa juu.

"Eneo la Ndagoni Wilaya ya Chakechake linakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi ambapo athari zake ni kubwa kiasi cha maeneo ya kilimo kuingiliwa na maji ya chumvi na wakulima kuachana na shughuli zao za asili," alisema.

Mwenyekiti wa kamati ya viongozi wakuu wa kitaifa, Machano Othman Said, aliwataka wananchi kuacha kukata miti aina ya mikoko inayostawi pembezoni mwa fukwe za bahari.

Alisema hivi sasa kumejitokeza kasi ya ukataji wa miti hiyo ambayo miongoni mwa sifa zake kubwa ni uwezo wa kuzuia kasi ya maji ya bahari kuingia katika makazi ya wananchi au mashamba. "Tumefanya utafiti na kubaini kwamba athari za mabadiliko ya tabianchi zipo, lakini kwa kiasi kikubwa zimesababishwa na tabia ya binadamu kukata miti ikiwamo mikoko ambayo hustawi vizuri pembezoni mwa bahari," alisema. Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, Suleiman Makame Ali, alisema baadhi ya maeneo ya Ndagoni wanayoishi watu wameanza kuyakimbia kutokana na athari za mabadiliko hayo.

# NEMC yaagizwa kuchangamkia fedha mradi mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu,**
NZEGA

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Chilo, ameliagiza Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), kuomba fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi wa kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi ili kutekeleza miradi itakayoondoa changamoto za maji kwa wakulima na wafugaji.

Alitoa agizo hilo jana ili kutekeleza mradi wa mabadiliko ya tabianchi katika Kijiji cha Ntoba, Kata ya Ndala, wilayani Nzega, mkoani Tabora, baada ya kutembelea miradi mingine wilaya za Bahi na Kongwa mkoani Dodoma iliyogharimu Shilingi bilioni tatu.

"Tunawaomba wenzetu wa NEMC wanaosimamia mradi huu waanze utaratibu wa kuomba fedha, waukamilishe ili uanze kutumika na wananchi kama ilivyokusudiwa kwenye shughuli za kilimo, mifugo na nyingine, mkaombe hizo fedha za mradi huu wa mabwawa yanayojumuisha wilayani Bahi na Kongwa, mkoani Dodoma," alisema.

Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Nzega alisema wilaya hiyo katika mkakati wa kutunza mazingira ipo kampeni ya kila mtoto anayezaliwa wilayani humo hupandiwa mti mmoja na wazazi wake ili kuhifadhi mazingira atakapokua akute mazingira salama.

"Kampeni hii maalumu ni endelevu ambayo tunataka kila mzazi wa mtoto anayezaliwa apandie mti wake kwa lengo la kuhifadhi mazingira yetu maana bila kuweka mikakati vizazi vijavyo vitakuta jangwa," alisema.

Miradi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa jamii za wakulima na wafugaji Wilaya ya Kongwa, Bahi na Nzega ilizinduliwa rasmi mwaka 2021 huku ikitarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu hadi mwaka 2024 kwa fedha za wahisani.



Wahitimu ngazi ya astashahada wakifurahia kuhitimu safari ya awali ya elimu ya masuala ya ardhi wakati wa mahafali ya 40 ya Chuo cha Ardhi Tabora. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Vijana wahimizwa kujiunga mafunzo ya skauti

**Na Christina Mwakangale**

WATANZANIA hasa vijana na watoto wametakiwa kujiunga na mafunzo na malezi ya skauti, yanayosaidia kundi hilo kuwa na makuzi na maadili mema kwenye jamii na kuwaepusha na vitendo viovu.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Kamishna Mkuu wa Chama cha Skauti Tanzania, Grace Kado, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya miaka minne katika uongozi wake.

Alisema kwamba kwa kipindi hicho, tangu mwaka 2018 hadi 2022, chama hicho kimefanikiwa kuongeza idadi ya wanachama kutoka 300,000 na kufikia 500,000 nchini.

"Ongezeko la wanachama kwenye skauti maana yake ni kwamba tumeongeza wigo wa kuwafikia Watanzania, hasa vijana. Chama bado kinahitaji mshikamano zaidi katika majukumu yake," alisema Kamishna Kado.

Pia alibainisha kuwa chama hicho hupata wanachama kutoka kundi la watoto wenye umri wa miaka mitano hadi wanaofikia kiwango cha veterani, ambao huimarisha mafunzo kwa wanachama wapya.

"Ninatangaza rasmi kumaliza muda wangu, kwa mujibu wa Katiba yetu ya mwaka 2017, Ibara ya 10.6 (8), na shughuli zote zitaelekezwa kwa Naibu Kamishna Mkuu, tukisubiria mlezi wetu, Rais Samia Suluhu Hassan kutukamilishia safu ya uongozi," alisema Kado.

"Wakati chama cha skauti kikifikisha miaka 100 tangu kienzishwe, tuhakikishe tunaendelea kuwa na mshikamano na kutoa elimu kwa makundi tofauti nchini, kwa lengo la kumkuza kijana kimaadili," alisema Kado.

Chama cha Skauti Tanzania malengo yake ni kuelimisha, kujitolea chenye malengo ya kumkuza kijana kiimani, kiakili, kijamii na kimwili kupitia shughuli mbalimbali kwa kutumia mbinu za kiskauti ili kuijenga dunia iliyo bora zaidi.

Kilianzishwa mwaka 1912 kikiwa na lengo la kumwandaa kijana kielimu ili aweze kujitegemea, kukabiliana na changamoto mbalimbali anazokumbana kwa kuzitatua na jamii husika.

# BAKWATA yaja na ufugaji nyuki kuepuka utegemezi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

BARAZA la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Singida limepanga kuanzisha miradi ya maendeleo ukiwamo wa ufugaji nyuki kwa lengo la kujikwamua kiuchumi na kuondokana na utegemezi wa kila kitu kutoka kwa wafadhili.

Shekhe wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro Issa, alibainisha kusudio hilo jana wakati wa kikao kazi kilichofanyika kwenye Msikiti Mkuu wa Taqwa, Manispaa ya Singida, kikiwashirikisha masheikh wa wilaya, wenyeviti wa BAKWATA wilaya na makatibu na kata.

Shekhe Issa alisema katika mradi wa nyuki, wamekubaliana kila kata itachangia Sh. 80,000 kwa ajili ya kununua mizinga ya nyuki 100 ambayo itawekwa eneo lenye ekari 464 lililoko Kata ya Misughaa, Wilaya ya Ikungi.

"Tumekubaliana tuanze na mradi huu wa nyuki kwa sababu unatoa tija haraka kwani ndani ya miezi sita tunaanza kuvuna asali na kimsingi mradi huu utawasaidia viongozi kupata kipato na kuendesha ofisi pasi na kutegemea wafadhili," alisema.

Shekhe Issa alisema waislamu wote mkoani Singida wanapaswa kujitokeza kuunga mkono miradi ambayo imepangwa kuanzishwa na BAKWATA ukiwamo umaliziaji wa ujenzi wa hospitali wilayani Iramba.

Pia alisisitiza suala la nidhamu kwa viongozi na waumini wote kuzingatiwa kwa kuwa jambo hilo limesisitizwa hata kwenye Katiba ya BAKWATA.

Mratibu wa Taifa wa BAKWATA Online Academy, Maadhi Abdulkarim, alisema kubuni miradi ya maendeleo kutaliwezesha baraza hilo kusonga mbele kiuchumi na kuufanya Mkoa wa Singida kuwa mkoa wa mfano nchini.

Abdulkarim ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Mufti (Mufti Development Fund), alisema heshima ya muumini ni kuwa na kazi inayomwingizia kipato kwa kuwa bila hivyo, hawezi kuheshimika na jamii.

"Uchumi unamwongezea mtu swawabu na heshima kwani umaskini siyo sifa na kiongozi mzuri ni lazima awe 'smart' zaidi kifkira na kiutendaji," alisema.

Aliongeza kuwa viongozi na waumini kwa ujumla lazima wafahamu kuwa nadharia ya kazi za uongozi ni kupanga, kuratibu, kuongoza na kudhibiti.

Mwenyekiti wa BAKWATA Wilaya ya Singida Vijijini, Issa Juma Mwiru, alisema mafunzo waliyopewa yatawafanya kubadilika kiutendaji na kubuni miradi ya maendeleo ambayo itawaingizia kipato.

HABARI KIMATAIFA

# Al-Shabab 30 wauawa Somalia

**MOGADISHU,** SOMALIA

JESHI la Marekani limesema shambulio la anga lililofanya kuwasaidia wanajeshi wa serikali nchini Somalia limewaua takribani wanamgambo 30 wa Kiislamu wa Al-Shabab.

Ilitajwa kuwa operesheni hiyo ilifanyika mwishoni mwa juma lililopita karibu na mji wa Galcad, kilomita 260 kaskazini mashariki mwa mji mkuu wa Mogadishu.

Katika siku chache zilizopita, jeshi la Somalia na wanamgambo wa Al-Shabab wamepigana kuudhibiti mji huo.

Kamandi ya Marekani barani Afrika ilisema, mashambulizi ya anga ya Ijumaa yalitokea, huku jeshi likishambuliwa na zaidi ya wanamgambo 100.

Wizara ya Habari ya Somalia ilisema, makumi ya wanamgambo hao waliuawa wakiwamo wengine saba baada ya kuvamia kambi ya kijeshi huko Galcad.

Al-Shabab imekuwa ikipambana na serikali kuu ya Somalia tangu mwaka 2006, kwa lengo la kulazimisha utawala wa Kiislamu wenye itikadi kali.

Wakati imesukumwa nje ya Mogadishu na maeneo mengine inaendelea kushambulia malengo ya kijeshi na ya kiraia.

Jumatatu iliyopita serikali ilisema jeshi lake na wanamgambo wa ndani wameuteka mji wa bandari wa Harardhere, ambao umekuwa kituo kikuu cha usambazaji cha Al-Shabab tangu 2010.

Katika ripoti yake kuhusu kundi la Galcad linalopigana na Kamandi ya Marekani ya Afrika ilisema magari matatu ya Al-Shabab yaliharibiwa na kamandi hiyo inatathmini kuwa hakuna raia aliyejeruhiwa au kuuawa.

Mtandao wa Al-Qaeda duniani ulitoa maelezo ambayo hayajathibitishwa na walengwa kuwa vikosi vya Kamandi ya Marekani Afrika vitaendelea kutoa mafunzo, kushauri na kuandaa vikosi vya washirika kusaidia kuwapa zana wanazohitaji kuishinda Al-Shabab.

**BBC**

# Russia, msaada silaha kwa Ukraine utazidisha vita

**MOSCOW,** RUSSIA

MSHIRIKA wa karibu wa Rais wa Russia Vladimir Putin, Vyaches-lav Volo-din amesema uwasilishaji wa silaha kwa Ukraine unaotishia usalama wa taifa lake utasababisha janga la kilimwengu na kusababisha pia majadiliano ya kutotumia silaha zinazoweza kuleta uharibifu mkubwa.

Mshirika huyo ambaye ni spika wa baraza la chini la bunge la Russia Duma, alionya kuwa usaidizi wa Marekani pamoja na Jumuiya ya kujihami NATO kwa Ukraine unaielekeza dunia katika vita vibaya.

Washirika wa Magharibi wa Ukraine, wiki iliyopita waliahidi msaada wa silaha wa mabilioni ya dola kwa taifa hilo, licha ya kushindwa kuishawishi Ujerumani kuondoa kura yao ya turufu, juu ya kutoa magari yao ya kivita yaliopo kwa washirika wa NATO yanayohitaji idhini ya Ujerumani ili kupelekwa nchini Ukraine.

**DW**

# IRGC yaionya EU kuwataja kama magaidi

**TEHRAN,** IRAN

JESHI la Walinzi wa Mapinduzi ya Kiislam Iran (IRGC) limeuonya Umoja wa Ulaya (EU) kuwaorodhesha kuwa ni magaidi, baada ya bunge la umoja huo wiki iliyopita kupiga kura na kuwaorodhesha kama magaidi.

Wabunge wa Bunge la Ulaya walipiga kura Jumatano wiki iliyopita kujumuisha IRGC kwenye orodha ya kigaidi ya mataifa 27 ya umoja huo kwa kuzingatia shughuli zake za kigaidi, ukandamizaji wa waandamanaji na upelekaji wake wa ndege zisizo na rubani kwa Russia.

Jeshi liliionya EU mwishoni mwa juma lililopita dhidi ya kufanya makosa kwa kuliorodhesha kama kundi la kigaidi, baada ya bunge la umoja huo kutaka hatua hiyo ichukuliwe.

Aidha, inatajwa kuwa kura hiyo haina nguvu kisheria lakini inakuja huku mawaziri wa mambo ya nje wa EU wakiwa wanatarajiwa kujadili kuimarisha vikwazo dhidi ya jamhuri hiyo ya Kiislamu wiki hii.

Kwa mujibu wa tovuti ya Guards' Sepah News, Mkuu wa IRGC Meja Jenerali Hossein Salami, katika matamshi yake ya kwanza juu ya hatua hiyo ya EU, alisema "Ikiwa wabunge hao wa Ulaya watafanya makosa, lazima wakubali matokeo".

"Unafikiri kwamba kwa kauli kama hizi inaweza kulitikisa jeshi hili kubwa, hatuna wasiwasi kamwe kuhusu vitisho kama hivyo au hata kuvifanya kazi, kwasababu kadri maadui zetu wanavyotupa nafasi ya kuchukua hatua, tunafanya kwa nguvu zaidi," alisema.

Walinzi hao wanasimamia kikosi cha kujitolea cha Basij, ambacho kimepelekwa kuzuia maandamano tangu katikati ya mwezi Septemba 2022 yaliyosababishwa na kifo cha Mahsa Amini (22), baada ya kukamatwa kwa madai ya kukiuka kanuni za mavazi za wanawake nchini Iran.

Mamlaka nchini Iran zinasema mamia ya watu, wakiwamo maofisa wa vikosi vya usalama wameuawa na maelfu kukamatwa katika ghasia hizo.

**VOA**




Maelfu ya Waisraeli wakiandamana huku wakionyesha mabango kushinikiza kusitishwa mageuzi ya mahakama kwa muungano unaotawala. **PICHA: EP**

# Waisraeli wapinga mageuzi ya mahakama

**TEL AVIV,** ISRAELI

TAKRIBANI watu 110,000 wamejazana katika mitaa ya Tel Aviv, katika mojawapo ya maandamano makubwa zaidi ya Israel dhidi ya serikali katika muongo mmoja uliopita.

Maandamano hayo yalienea katikati mwa jiji huku mabango yakipandishwa yakitaka kusitishwa kwa muungano unaotawala, ambao ni wenye siasa kali za mrengo wa kulia na utaifa wa kidini katika historia ya Israel.

Yaara Ben Geraluf, mwalimu kutoka Jaffa, kitongoji cha magharibi mwa pwani, akizungumza na BBC aliitaja serikali yake kuwa ni hatari, "Serikali hii haitakuwa nzuri kwa wanawake, watu maskini na bila shaka kwa Wapalestina".

Waandaaji wanasema wanajaribu kusitisha mapinduzi yanayofanyika dhidi ya mfumo wa serikali, huku ikielezwa kuwa ni wiki ya pili ambayo maandamano makubwa yamefanyika katika miji minne tofauti.

Kiongozi wa upinzani Yair Lapid alihutubia umati wa watu mjini Tel Aviv, akisema watu wanaopenda nchi walienda kutetea demokrasia yake na mahakama zake, huku akisisitiza kuwa hawatakata tamaa hadi washinde.

Hatua hii inakuja wiki tatu baada ya Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu kurejea madarakani na kuunda muungano wa kwanza imara wa Israel katika kipindi cha miaka mitatu.

Alisema Waisraeli walipigia kura serikali kamili ya mrengo wa kulia na usalama.

Inabainishwa kuwa waandamanaji wanamshutumu Netanyahu kwa kutishia utawala wa kidemokrasia, huku kukiwa na mzozo ambao haujawahi kushuhudiwa kati ya serikali mpya na majaji wa Israel.

Marekebisho yaliyopangwa ya muungano huo yangeiruhusu kubatilisha mahakama ikiwa itafutilia mbali sheria zijazo.

Wapinzani wanasema hiyo inatishia mfumo wa kidemokrasia wa Israeli wa kuangalia na kusawazisha.

Wakosoaji pia wanasema Netanyahu, ambaye yuko katika kesi ya ufisadi, anajaribu kuwadhibiti majaji katika jaribio la mwisho la kukwepa kufungwa jela.

**BBC**

# AZAM YAMREJESHA EDINHO IVORY COAST KWA MKOPO

**Na Saada Akida**

Azam FC, imemtoa kwa mkopo mshambuliaji wao, Tape Edinho, kwenda Klabu ya Stella Club d'Adjame ya Ivory Coast kuitumikia kwa kipindi cha miezi sita.

Edinho aliyesajiliwa kwa mkataba wa miaka miwili na Azam FC katika usajili wa dirisha kubwa, ametolewa kwa mkopo ili kutoa nafasi kwa kipa raia wa Ghana, Abdulai Iddrisu, aliyejiunga na klabu hiyo katika kipindi cha dirisha dogo kwa ajili ya kukiimarisha timu hiyo katika michezo iliyopo mbele yao, Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la Shirikisho (FA Cup).

**Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Thabiti Zakaria 'Zaka Zakazi', alisema kwa sababu ya Kanuni ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kila klabu kutakiwa kusajili idadi ya wachezaji wakigeni wasiozidi 12, wameamua kumtoa Edinho kwa mkopo ili kumpa nafasi kipa huyo.**

Alisema kwa kuzidi mchezaji mmoja wanalazimika kumtoa kwa mkopo mshambuliaji huyo kwenda nyumbani kwao kuitumikia Stella Club d'Adjame.

"Tukumbuke dirisha dogo tumesajili kipa kutoka nchini Ghana (Iddrisu), uwapo wa nyanda huyo unafanya timu yetu wachezaji wa kigeni kuwa 13, lazima mmoja aondoke twende sawa na Kanuni ya TFF, tumemtoa kwa mkopo Tape kwa muda wa miezi sita baadaye atarejea katika klabu yake ya Azam FC," alisema Zakazi.

Alisema wamelazimika kufanya usajili wa kipa na kupunguza mchezaji wa ndani kwa sababu nafasi walioongeza mtu ilikuwa na shida na wanaimani kipa huyo atasaidia timu hiyo kufikia malengo yake.

Zakazi alisema matarajio yao makubwa ni kuhakikisha wanamaliza nafasi tatu za juu katika ligi pamoja na kufanya vizuri katika Kombe la FA kwa kufuzu hatua ya 32 na kutwaa taji hilo.

Azam kwa sasa ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na alama 43, nne nyuma ya Simba iliyoko nafasi ya pili na 10 nyuma ya vinara wa ligi hiyo, Yanga.

**SHUTI...**




Winga mpya wa Chelsea aliyesajiliwa katika usajili wa dirisha dogo Januari hii, Mykhailo Mudryk, akijaribu kuachia shuti huku beki wa Liverpool, James Miller, akijipanga kuzuia, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Anfield na kumalizika kwa sare tasa juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Championship ni vita kupanda Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

KUMEKUWA na vita kali kwa timu za Ligi ya Championship zikipigania vikumbo kupanda Ligi Kuu msimu ujao ambapo juzi ligi hiyo iliingia raundi ya 16, vinara JKT Tanzania wakizidi kuonyesha kuwa safari hii wamepania kurudi, waliposhinda ugenini mabo 3-2 dhidi ya Copco.

Mechi hiyo ilichezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza na kuwafanya maafande hao kufikisha pointi 37 wakiendelea kutesa kileleni, huku wapinzani wao kwenye vita hivyo, Kitayosce wakiangukia pua baada ya kutandikwa mabao 2-1 dhidi ya Pan African, mechi ikipigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Kutokana na kipigo hicho, Kitayosce inabaki na pointi zake 35, ikizidiwa alama mbili na vinara JKT Tanzania, huku ikisalia kwenye nafasi ya pili ya msimamo wa ligi hiyo.

Pamba, timu kongwe nchini, imekwea hadi nafasi ya tatu ikifikisha pointi 31, baada ya kuidungua KenGold bao 1-0, mechi ikichezwa Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga mkoani Rukwa, ikifufua matumaini ya kupanda moja kwa moja Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, au kwenda kwenye mechi za mchujo kuisaka nafasi hiyo.

Mbuni FC, timu ambayo iliongoza Ligi ya Championship kwa raundi kadhaa za mzunguko wa kwanza, hivi sasa imeonekana kuchoka, kwani juzi pia ilipata kipigo cha mabao 2-1 kwa timu inayoonekana kuwa dhaifu kwenye ligi hiyo, Ndanda FC, mechi likipigwa Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara.

Matokeo hayo yamezidi kuiondolea matumaini Mbuni FC ya kupanda moja kwa moja Ligi Kuu, kwani imeshuka hadi nafasi ya sita ikiwa na pointi 24.

Timu ya Biashara United ikiwa kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara, iliiadhibu Fountain Gate bao 1-0, matokeo ambao yameishusha hadi nafasi ya nne timu hiyo inayotabiriwa kupanda Ligi Kuu msimu ujao.

## Polisi FC bado yajipa matumaini Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa timu ya Polisi FC, Yusuf Sape, amesema licha ya kuanza vibaya katika michezo miwili ya mzunguko huu wa lala salama Ligi Kuu Zanzibar, kikosi chake kimeimarika ikilinganishwa na mzunguko wa kwanza.

Timu ya Polisi imeambulia sare katika michezo miwili ya mzunguko huu wa pili huku ikiendelea kubaki katika mstari wa hatari wa kushuka daraja.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema wanahitaji kupata alama tatu kwa kila mchezo uliobaki ili kuinusuru timu hiyo kushuka daraja.

Alisema upo uwezekano mkubwa wa timu hiyo kujinusuru kutokana na jitihada wanazoonyesha wachezaji wake wawapo uwanjani na kwamba kupata sare katika michezo miwili ya mwanzo si matokeo mabaya kwani timu zote za Ligi Kuu zina nguvu na ari ya kusaka ushindi baada ya mapumziko waliyoyapata.

"Kwa mwenendo wa Ligi tunavyoenda nayo basi ukipata alama moja hili si jambo baya, kwa sababu timu zote zinacheza kwa nguvu na wachezaji bado hawajachoka kwa kuwa wametoka katika mapumziko, hivyo tunaimani mchezo wetu ujao tutapata alama tatu," alisema na kuongeza kwa sasa wanajiandaa na mechi ijayo dhidi ya Taifa Jang'ombe.

Timu ya Polisi FC ipo nafasi ya 14 katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 13 katika michezo 18 iliyocheza.

## Simbu asifu vipaji riadha wanawake

**Na Shufaa Lyimo**

MWANARIADHA mwenye sifa ya kuipeperusha vema bendera ya Tanzania kimataifa, Alphonce Simbu, ameeleza kubaini vipaji vingi kupitia mashindano ya wanawake ya mchezo wa riadha (Ladies First), ambayo yamemalizika Dar es Salaam jana.

Akizungumza na gazeti hili jana jijini Dar es Salaam jana, Simbu alisema Tanzania ina wanariadha wengi chipukizi ila tatizo wanashindwa kutoka kutokana na kukosekana kwa wawezeshaji.

"Mashindano haya yanaushindani, kila mchezaji ameonyesha kipaji chake, ninaamini mashindano yajayo tutapata wanariadha ambao watashiriki mashindano mengine makubwa," alisema Simbu.

Aidha, alisema wanawake wakiwezeshwa wanaweza na kuwataka wazazi kuruhusu watoto wao wa kike wajitokeze kwenye michezo.

Mashindano hayo yalishirikisha mikoa 31 kutoka Tanzania Bara na Visiwani ambapo wanariadha 186 walishiriki kwenye mbio kuanzia mita 100 hadi10,000.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### JUDE KUKATAA OFA

KIUNGO wa kati wa England, Jude Bellingham, anatarajiwa kukataa ofa ya mkataba mpya kutoka kwa Borussia Dortmund, huku Manchester City wakihisi kuwa wanaongoza katika harakati za kumsajili kinda huyo mwenye umri wa miaka 19. (***Star***)

### CHELSEA NA CAICEDO

CHELSEA wanajipanga kuongeza ofa yao kwa kiungo wa Ecuador, Moises Caicedo, karibu na pauni milioni 65 ambazo zinaweza kuishawishi Brighton kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. (***Mirror***)

### ZIYECH KUBADILISHWA

CHELSEA pia itakuwa tayari kubadilishana winga wa Morocco, Hakim Ziyech, mwenye umri wa miaka 29 na kiungo wa kati wa Barcelona na Ivory Coast, Franck Kessie, mwenye umri wa miaka 26. (***Sport***)

### GARNACHO ATAKIWA KUSAINI

KLABU ya Manchester United inataka mshambuliaji wa Argentina, Alejandro Garnacho, kutia saini mkataba mpya wa miaka nane, lakini wawakilishi wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 hawataki. (***Mirror***)

### VLAHOVIC APEWA OFA

KLABU ya Manchester United imetoa ofa kwa mshambuliaji wa Juventus, Dusan Vlahovic, huku Arsenal, Chelsea, Paris St-Germain na Bayern Munich pia zikimwania mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia mwenye umri wa miaka 22. (***90 min***)

### ZANIOLO AWINDWA WEST HAM

KLABU ya West Ham imetoa ofa ya kumnunua kiungo wa kati wa Italia, Nicolo Zaniolo, iliyokataliwa na AS Roma, huku mazungumzo ya kumnasa mchezaji huyo wa miaka 23 yakiendelea. (***Calciomercato***)

### DEULOFEU ANYATIWA ROMA

AS Roma itamnunua mshambuliaji wa Udinese, Gerard Deulofeu mwenye umri wa miaka 28 mara watakapomtoa Nicolo Zaniolo. (***Calciomercato***)

### ENRIQUE ATAKIWA BRAZIL

KOCHA wa zamani wa Hispania, Luis Enrique mwenye umri wa miaka 52, ni mmoja wapo wa chaguzi zinazofikiriwa kuchukua nafasi ya kocha mpya wa Timu ya Taifa ya Brazil. (***UOL Esporte***)

### CAMAVINGA AZUIWA ARSENAL

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesema kiungo wa kati wa Ufaransa, Eduardo Camavinga, mwenye umri wa miaka 20, ambaye amekuwa akihusishwa na Arsenal, hataruhusiwa kuondoka katika klabu hiyo ya Hispania. (***Mail***)


### GUNDOGAN AWANIWA BARCA

KLABU ya Manchester City ipo kwenye mazungumzo na kiungo wa kati wa Ujerumani, Ilkay Gundogan, ambaye amekuwa akihusishwa na Barcelona kuhusu kuongeza mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32. (***Athletic***)

### MAJER AFUATILIWA UNITED

KLABU za Manchester United na Tottenham Hotspur zote zinamfuatilia kiungo wa kati wa Rennes na Croatia, Lovro Majer, mwenye umri wa miaka 25. (***Jeunes Footeux***)

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: HAKUNA NAFASI MAN CITY KUIZUIA ARSENAL

●●● Hata kama watapoteza dhidi ya Man United, ikiwa tutacheza hivi hatutawakamata, lazima sasa...

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amewaonya wachezaji wake wa Manchester City kwamba, hakuna "nafasi" ya wao kuwanasa vinara wa Ligi Kuu England Arsenal kama hawataboresha kiwango chao.

City wamepoteza pointi nane katika mechi zao sita zilizopita za Ligi Kuu na wamepitwa na Arsenal kwa pointi tano, wakiwa wamecheza mchezo mmoja zaidi.

**Na jana Jumapili Arsenal walikuwa wanacheza na Manchester United na Guardiola alisema hata kama watapoteza, lakini wao hawana nafasi ya kuwapiku kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu.**

"Man City haina nafasi hiyo," alisema akiwaambia waandishi wa habari. "(Hata kama) watapoteza dhidi ya Man United, ikiwa tutacheza hivi hatutashinda, hatutawakamata. Lazima tubadilike sisi wenyewe.

"Sikiliza, sisi ni wa pili kwenye msimamo," aliongeza. "Hatuko nyuma ya Arsenal kwa pointi 25, bado tupo. Ni pointi 57 bado kucheza."

Lakini kuhusu kama bado wanaweza kushinda taji la msimu huu, Guardiola alijibu: "Kwa njia hii, hakuna nafasi. Tuna Kombe la FA, tuna Ligi ya Mabingwa Ulaya, nafasi ni finyu."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
YOUNG AFRICANS
VERSUS
RUVU SHOOTING
1 | 1.08
X | 4.48
2 | 13.05

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# UNITED YAJITOSA KWA VLAHOVIC

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Dusan Vlahovic, amepewa ofa kutoka Manchester United, kwa mujibu wa 90mins.

Vlahovic alijiunga tu na Juventus kutoka Fiorentina Januari iliyopita kwa mkataba wa miaka minne, lakini anaweza kuwa tayari kuhama.

Hiyo ni sehemu ya msukosuko kutoka kwa wababe hao wa Serie A huku wakikatwa pointi 15 kwa madai ya makosa ya kifedha na uhasibu.

Juventus itakata rufani dhidi ya uamuzi wa mahakama, lakini inawaacha katika vita tayari wakiwa wameshuka hadi nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Italia, na ripoti zinaonyesha kuwa watakuwa na kibarua kigumu kuwashikilia baadhi ya wachezaji wao muhimu.

Arsenal, Chelsea, Paris Saint-Germain na Bayern Munich pia wameonyesha nia ya kumtaka Vlahovic.

Kucheza soka ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ndio malengo ya mshambuliaji huyo wa Serbia.

Hadi sasa amefunga mabao 16 katika mechi 36 alizoichezea Juventus na klabu hiyo inaelewa nafasi ya mchezaji huyo na anaweza kuuzwa Januari hii au mwishoni mwa msimu huu.

# Lampard akalia kuti kavu Everton

**LONDON,** England

MMILIKI wa Everton, Farhad Moshiri, amesema uamuzi kuhusu mustakabali wa kocha Frank Lampard hauko kwake.

Moshiri, ambaye ameajiri makocha sita wa kudumu tangu alipowekeza katika klabu hiyo mwaka 2016, alikuwapo uwanjani wakati Everton ikifungwa mabao 2-0 na West Ham Jumamosi kwenye Uwanja wa London.

Hicho kilikuwa kipigo cha nane katika mechi tisa kwa Everton katika mashindano yote na kuwaacha nafasi ya 19 kwenye msimamo, wakiwa pointi sawa na Southampton iliyo nafasi ya mwisho.

Hata hivyo, Moshiri ambaye alimuunga mkono hadharani Lampard kabla ya kufungwa na Southampton wiki iliyopita, alidai uamuzi kuhusu kocha huyo hauko mikononi mwake.

"Siwezi kutoa maoni. Si uamuzi wangu," alisema akiambia Sky Sports.

Bill Kenwright Mwenyekiti wa Everton, pia aliulizwa ikiwa muda ulikuwa umekwisha kwa Lampard alijibu kuwa yeye hana majibu.

"Yamekuwa matokeo mabaya kwetu sote na kwa Frank," alisema. "Lakini siwezi kukuambia kwamba muda wake umekwisha."

Moshiri alisema katika mahojiano na talkSPORT mapema mwezi huu awali alifanya maamuzi juu ya uteuzi wa makocha kutokana na matakwa ya mashabiki.



CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# KOCHA PRISONS ALIA NA 'MIPIRA ILIYOKUFA'

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupokea kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Ihefu juzi kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Kocha Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shasaban Mtupa, amesema wachezaji wake hawakuwa makini kuzuia faulo za wapinzani wao na ndizo zilizowahukumu kupoteza mechi hiyo.

"Tumehukumiwa na 'mipira iliyokufa', tumepoteza mchezo huu, lakini inaumiza kwa sababu ukiangalia mechi ilionekana ni yetu kabisa huu, kwanza tuliruhusu bao la mapema likatutoa mchezoni, tukarudisha kwa mkwaju wa penalti, lakini tukafanya kosa kama la kwanza.

"Siku za nyuma tulikuwa na makosa kama haya, lakini tukayarekebisha, yakaonekana yamepungua, lakini kama yanarudi tena, mwisho wa siku tunarudi kwenye uwanja wa mzoezi ili kufanyia kazi tuwe bora," alisema Mtupa.

Prisons ilijifunga yenyewe bao la kwanza dakika ya pili tu ya mchezo, kupitia kwa beki wake, Ezekia Mwashilindi, alipojaribu kuokoa faulo ya Never Tegere, lakini ilirudisha bao kwa mkwaju wa penalti wa Jeremiah Juma dakika ya 72, kabla ya Rafael Daudi kupachika la pili dakika ya 90, akiunganisha kona ya Tegere.

Kocha Mkuu wa Ihefu, Zuberi Katwira alisema kwa hali ilivyofika sasa wanatakiwa kutafuta pointi tatu nyumbani na ugenini ili kujiweka salama kwenye msimami wa Ligi Kuu

"Tumeshinda kwenye mechi ngumu kama hii na hali ya mvua, ilikuwa ni kujitahidi tu kutofanya makosa, Prisons ni timu ngumu kuifunga kwenye uwanja wake wa nyumbani, kazi kubwa sana imefanyika, niwapongeze wachezaji wangu wametumia nafasi zilizopatikana.

"Kwa sasa tunatafuta pointi tatu sehemu yoyote iwe nyumbani au ugenini kwa sababu tunazihitaji ili kutuweka sehemu salama," alisema.

Kwa ushindi huo, Ihefu ilipanda hadi nafasi ya 10 kabla ya mechi za jana, ikiwa na pointi 23 kwa mechi 21 ilizocheza huku Prisons ikishika nafasi ya 13, pointi zake 21 kwa mechi 21 pia.

HAMNIWEZI...



Mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland, akiwatoka mabeki wa Wolverhampton Wanderers, kabla ya kuifungia timu yake bao la kuongoza katika dakika ya 40, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Etihad jana.

# *Yanga kuivaa Ruvu na majembe mapya*

INATOKA UK 24

ina wachezaji wazuri, lakini hilo halijalishi zaidi ya kusaka pointi tatu muhimu.

Alisema wameiangalia Yanga mechi zote na wameona ubora wa wapinzani wao hao, hivyo wataingia uwanjani kwa tahadhari kubwa kwenda kupambana kupata matokeo.

"Tumejipanga vizuri, tayari tumeweka mikakati yetu ya kujinasua katika nafasi ya kushuka, tunaitaka sana hii mechi, kwa sababu tunahitaji matokeo kwa mbinu zetu tunaenda kupata pointi muhimu.

"Tumechukua tahadhari zote kwa sababu Yanga mechi kadhaa wanashindwa kupata matokeo kipindi cha kwanza na kufurahi ushindi kipindi cha pili, hilo tumeliona na tumefanyia kazi na tunaingia na mbinu tofauti," alisema Msese.

Alisema wanaingia katika mchezo huo wa mikakati ya kusaka ushindi na alama tatu na sio kucheza kwa kuwafurahisha watu.

Yanga ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 53, sita mbele ya Simba iliyopo nafasi ya pili na 10 mbele ya Azam FC inayoshika nafasi ya tatu. Kwa upande wa Ruvu Shooting, yenyewe inaburuza mkia ikiwa na alama 14, baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 20.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 23/01/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2095 | Persis Solo vs PS Tni | 1.96 | 3.17 | 3.64 |
| 15:20 | 1689 | AL Qaisoma vs AL Khlood | 2.60 | 2.65 | 2.70 |
| 15:45 | 1448 | Aswan vs Ismaily SC | 2.73 | 2.93 | 2.73 |
| 15:45 | 3707 | Farco FC vs Enppi Club | 2.83 | 2.88 | 2.68 |
| 16:00 | 5578 | Singida BS FC vs Azam | 2.54 | 2.40 | 2.03 |
| 16:15 | 1126 | Al Dhafra vs Dibba Al Fujairah | 2.09 | 3.36 | 3.10 |
| 16:15 | 1951 | Ajman Club vs Shabab AL Ahli Dubai Club | 3.68 | 3.62 | 1.81 |
| 16:30 | 1362 | Al Kuwait SC vs AL Tadamon | 1.60 | 3.56 | 5.16 |
| 16:30 | 2557 | Al-Shamal vs Lekhwiya SC | 7.45 | 5.18 | 1.29 |
| 16:30 | 2751 | AL Nasr vs Al Jahra | 2.50 | 3.05 | 2.69 |
| 16:30 | 3068 | Kenkre FC vs Sreenidi Deccan FC | 5.40 | 3.79 | 1.54 |
| 17:45 | 3999 | Muharraq SC vs Al Ahli Manama | 1.49 | 3.71 | 6.19 |
| 18:00 | 1708 | Aris Limassol vs Apollon Limassol | 2.34 | 3.25 | 2.98 |
| 18:00 | 3087 | Chindia Targoviste vs Argesul Pitesti | 2.15 | 2.97 | 3.60 |
| 18:00 | 4140 | Manama Club vs AL Khalidiyah | 2.30 | 3.01 | 3.01 |
| 18:00 | 4349 | Markez Balata vs Thagafi Tulkarem | 2.09 | 3.12 | 3.33 |
| 18:00 | 4653 | Shabab AL Khaleel vs Hilal Al-Quds | 2.02 | 3.16 | 3.47 |
| 18:00 | 4675 | Jabal EL Mokaber vs Shabab Alsamu | 1.37 | 4.46 | 6.85 |
| 18:00 | 5499 | Ceramica Cleopatra vs Talaea El Gaish | 2.08 | 3.08 | 3.72 |
| 19:00 | 1657 | Young Africans vs Ruvu Shooting | 1.08 | 4.48 | 13.05 |
| 19:00 | 5103 | Baniyas vs AL Wahda Scc (UAE) | 3.32 | 3.53 | 1.94 |
| 19:00 | 5740 | Al Arabi Doha SC vs Al Sadd SC | 2.90 | 3.83 | 2.03 |
| 20:00 | 1271 | El Ittihad Alexandria vs Haras EL Hodood | 1.76 | 3.28 | 4.97 |
| 20:00 | 1395 | Konyaspor vs Ankaragucu | 1.98 | 3.44 | 3.59 |
| 20:00 | 1641 | Hapoel Ramat Gan vs Ironi Tiberias | 4.05 | 3.46 | 1.87 |
| 20:00 | 3257 | Anorthosis Famagusta vs EN Paralimni | 1.66 | 3.78 | 4.90 |
| 20:00 | 3311 | Umraniyespor vs Fenerbahce | 5.29 | 4.18 | 1.55 |
| 20:00 | 4271 | Hapoel Afula vs AS Ashdod | 1.69 | 3.15 | 4.30 |
| 20:00 | 5052 | Hapoel Petah Tikva vs Maccabi Petach Tikva | 2.72 | 2.99 | 2.72 |
| 20:00 | 5187 | Caykur Rizespor vs Denizlispor | 1.46 | 4.14 | 5.79 |
| 20:15 | 2111 | Al Shabab Kuwait vs Al Salmiyah | 5.79 | 4.14 | 1.46 |
| 20:30 | 1268 | Bologna vs Cremonese | 1.88 | 3.32 | 4.07 |
| 20:30 | 4399 | Sedan vs Le Mans | 2.45 | 3.24 | 2.72 |
| 20:45 | 1896 | Al Hidd Club vs Bahrain Club | 2.14 | 3.06 | 3.27 |
| 21:00 | 1078 | Duisburg vs Waldhof Mannheim | 2.58 | 3.27 | 2.58 |
| 21:00 | 3472 | Farul Constanta vs CFR Cluj | 2.96 | 2.96 | 2.47 |
| 21:00 | 3527 | SCU Torreense vs CD Feirense | 2.60 | 3.00 | 2.73 |
| 21:00 | 3832 | Santa Cruz RN vs Forca E Luz RN | 1.50 | 4.16 | 5.20 |
| 21:30 | 2454 | Maccabi Tel Aviv vs Maccabi Haifa | 2.27 | 3.25 | 2.84 |
| 22:00 | 1873 | Jong AZ Alkmaar vs Helmond Sport | 1.79 | 3.68 | 3.94 |
| 22:00 | 1874 | Sudan vs Madagascar | 3.54 | 2.89 | 2.26 |
| 22:00 | 4242 | Jong Ajax vs Roda Kerkrade | 2.73 | 3.47 | 2.32 |
| 22:00 | 5543 | Jong PSV vs VVV Venlo | 2.23 | 3.52 | 2.84 |
| 22:45 | 3374 | US Pays de Cassel vs Paris St Germain | 24.68 | 14.81 | 1.03 |
| 22:45 | 4176 | Darvel FC vs Aberdeen | 22.73 | 7.44 | 1.09 |
| 22:45 | 5696 | Inter vs Empoli | 1.26 | 5.55 | 9.51 |
| 23:00 | 3398 | Fulham vs Tottenham | 3.08 | 3.63 | 2.09 |
| 23:00 | 3969 | FC Andorra vs Albacete Balompie | 2.03 | 3.12 | 3.76 |
| 23:00 | 4119 | Valencia vs Almeria | 1.59 | 4.00 | 5.21 |
| 23:15 | 2397 | Boavista vs GD Chaves | 2.26 | 3.24 | 3.09 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Nipashe Jumatatu Januari 23, 2023




Guardiola: Hakuna nafasi City kuizuia Arsenal

UKURASA 21



Mshambuliaji mpya wa Yanga, Kennedy Musonda, anatarajiwa kuanza leo dhidi ya Ruvu Shooting.

# Yanga kuivaa Ruvu na majembe mapya

## ●●● Mamadou naye ndani, Nabi awaita mashabiki kwa Mkapa leo kushuhudia...

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga leo ikishuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha Ruvu Shooting kwenye mechi ya Ligi Kuu raundi ya 21, Kocha Mkuu wa vinara hao, Nasreddine Nabi, amesema ataangalia uwezekano pia wa kumpa nafasi beki mpya wa timu hiyo raia wa Mali, Mamadou Doumbia, aliyesajiliwa katika usajili wa dirisha dogo Januari hii.

Katika mchezo huo kila timu inahitaji pointi kwa lengo la kujiimarisha, Yanga wakihitaji alama hizo kujihakikisha kuendelea kukaa kileleni mwa msimamo huku Ruvu Shooting wakitaka kujinusuru kushuka daraja.

Ruvu Shooting wanashuka dimbani kukabiliana na Yanga wakitoka kupata sare tasa dhidi ya Coastal Union, ambayo ilikuwa mwenyeji wa mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga. Kwa upande wa Yanga, yenyewe ilishinda mabao 2-1 dhidi ya Ihefu FC, katika mechi iliyopita kwenye uwanja huo.

Kuelekea mchezo huo Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema walikuwa na wiki nzuri ya kufanya maandalizi kuliko siku zilizopita kwa sababu wamefanya kazi nzuri kwa kujiandaa na mechi hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaze alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu ya nafasi waliyopo Ruvu Shooting, lakini kutokana namna ulivyo hutoa ushindani mkubwa wanapokutana na Yanga.

"Tumefanya maandalizi mazuri ukizingatia Ruvu Shooting hawako katika nafasi nzuri kwenye msimamo, ninaamini mchezo utakuwa wa ushindani kwa sababu tunahitaji kupata pointi na wapinzani wetu nao wanahitaji alama kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo.

"Tunahitaji kufanya vizuri na kusaka pointi tatu muhimu kwa sababu zinatusogeza kufika katika nchi ya ahadi, kwetu ni kutetea ubingwa wetu," alisema Kaze.

Alisema wanatarajia kutumikia nyota wao mpya, Mamodou ambaye kila kitu kuhusu kibali kimekamilika na sasa wanaangalia jinsi ya utayari wake wa kucheza katika mchezo huo wa leo.

"Hizi mechi za mwisho zinakuwa na presha kubwa kwa sababu kila timu inahitaji kufanya vizuri na kupata alama tatu muhimu, tunalazimika kucheza kama fainali ili kusaka pointi tatu muhimu," alisema Kaze.

Mwakilishi wa wachezaji wa Yanga, Clement Mzize, alisema wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanapambana kusaka pointi muhimu kwa kuyahamisha yale waliyopewa mazoezi na kuyapeleka katika mechi.

"Kuhusu ushindani wa namba katika kikosi cha Yanga upo, hivyo kinachotakiwa ni kuonyesha kiwango kizuri ili kulishawishi benchi la ufundi kunipa nafasi, lakini nawaheshimu sana Fiston Mayele na Kennedy Musonda," alisema Mzize.

Kocha Msaidizi wa Ruvu Shooting, Frank Msese, alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu Yanga

INAENDELEA UK 23

## Azam yamrejesha Edinho Ivory Coast

UKURASA 20

**Na Saada Akida**

Azam FC imemtoa kwa mkopo mshambuliaji wao, Tape Edinho, kwenda Klabu ya Stella Club d'Adjame ya Ivory Coast kuitumikia kwa kipindi cha miezi sita.

Edinho aliyesajiliwa kwa mkataba wa miaka miwili na Azam FC katika usajili wa dirisha kubwa, ametolewa kwa mkopo ili kutoa nafasi kwa kipa raia wa Ghana, Abdulai Iddrisu, aliyejiunga na klabu hiyo katika kipindi cha dirisha dogo kwa ajili ya...



## Mabeki wa5 kikwazo kwa Ronaldo nyavuni

UKURASA 12

**LONDON, England**

CRISTIANO Ronaldo anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora katika zama za kisasa. Rekodi ya Ronaldo inajieleza yenyewe jinsi nyota huyo wa Ureno alivyo mmoja wa wachezaji bora zaidi kuwahi kutokea duniani.

Ronaldo pia amebadilisha mchezo wake sana ili kukabiliana na umri. Alianza uchezaji wake kama winga mwenye kasi ambaye angeweza kufanya fujo dhidi ya safu...



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >